# Mwongozo kwa Waalimu

## Wakati na Biblia Daraja la tatu na la nne

Mfululizo wa B
Somo la kwanza hadi la sita

www.besweb.com

## Bible Educational Services

Registered Charity UK (No 1186004)
Imesajiliwa kama shirika la Hisani Uingereza (Namba 1186004)

**Dhamira**
Kuandaa masomo ya Biblia kwa ajili ya wadau ili kutumika kuwakilisha kweli ya Yesu Kristo kwa kizazi kijacho ulimwenguni kote.

**Maono**
Kufikia kizazi kijacho kwa lugha zao kwa kutumia mtaala wetu kamili kwa kukuza na kusaidia mtandao wa kimataifa wa wabia wanaojitolea.

## HABARI KWA UJUMLA

**Bible Educational Services hufanya nini:**

Bible Educational Services (BES) huchapisha masomo ya Biblia ya "Wakati na Biblia/Bibletime", "Maisha Mapya/New Life" na "Wakusanyaji/Gleaners" kwa Lugha ya Kiingereza na kusaidia vituo vya Shule ya Biblia kwa njia ya Posta pamoja na mashirika mengine ya namna hiyo yanayotumia masomo ya BES huko Uingereza na nchi zingine. BES hufanya hivi kwa kutembelea, kutoa ushauri, kutoa mafunzo na kuunganisha mashirika haya na mengine. Sasa hivi, BES inafanya kazi na vikundi mbalimbali kutoka nchi zingine, vinavyohusika na kutafsiri, kubuni, kuchapisha na kusambaza masomo. Masomo haya yanatolewa bure kabisa kwa kila mtoto.

Kwa mara ya kwanza, masomo ya Wakati na Biblia yalitumika huko Kusini mwa Ireland (Uingereza) miaka sitini iliyopita. Bible Educational Services (BES) wamechukua jukumu la uhariri wa masomo ya Wakati na Biblia kwa lugha ya Kiingereza na Lugha zingine. Kwa muda mrefu, Masomo ya Wakati na Biblia (Bibletime) yalichapishwa kwenye muundo wa A4 ambao uliwawezesha wanafunzi kutoka baadhi ya maeneo kutuma masomo yao kwenye kituo cha BES kwa ajili ya kusahihishwa kila baada ya wiki nne. Hivi karibuni, masomo ya miezi sita yamechapishwa kwa muundo wa A5. Muundo huu umefanya utumiaji wa masomo haya uwe rahisi na wakufaa zaidi kwa makanisa na shule ambazo hazina ufanisi mzuri wa mfumo wa njia ya posta. Tunawashukuru Every Home Crusade au Revival Movement huko Belfast Uingereza kwa kutuwezesha kufanya hivi.

Masomo ya BES ni ya kipekee kwa sababu yameandaliwa na vikundi mbalimbali kutoka makanisa na shule mbalimbali ambavyo vimezingatia mtaala (Syllabus). Masomo yamepangiliwa vizuri na yanamruhusu mwanafunzi kuyatumia kwa muda mrefu hadi atakapotimiza umri wa miaka ishirini. Masomo yanapatikana katika madaraja matano ambayo yamezingatia umri tofauti. Nayo ni, masomo kwa ajili ya watoto wa chekechea (chini ya miaka mitano), miaka mitano hadi saba, miaka nane hadi kumi, miaka kumi na moja hadi kumi na mitatu na miaka kumi na minne hadi kumi na sita. Kuna Mtaala wa miaka mitatu katika kila kikundi cha umri (angalia ukurasa wa 6). Vikundi hivi vya umri vinaweza kutofautiana kulingana na uwezo tofauti wa watoto. Rasilimali na masomo ya Wakati na Biblia yanawapa watoto fursa ya kujifunza Neno la Mungu, kujifunza Habari za Biblia na kujifunza kukabiliana na changamoto zinazotokea maishani mwao kulingana na mwongonzo wa Injili ya Bwana Yesu Kristo.

Nakala zilizochapishwa za masomo kwa Lugha ya Kiingereza zinapatikana kwenye tovuti ya BES /BES website – www.besweb.com au kwa katibu ofisi ya BES Uingereza. Yanapatikana pia kwa lugha zingine kwenye tovuti. Kwenye tovuti kuna nyaraka muhimu kwa mtu yeyote au shirika linalopenda kushirikiana nasi.

## Anuani za mawasiliano za BES

**Ofisi ya Uingereza (Northern Ireland) (Mhifadhi wa masomo yote ya Kiingereza)**
37a Belmore Street, Enniskillen, Northern Ireland BT74 6AA
Simu: +44 286 632 2462

**Katibu wa Uingereza**
Bw. Stephen Gillham,
Barua pepe: stephen.gillham@besweb.com

Tovuti: www.besweb.com
Barua pepe: info@besweb.com

**Mshirika Tanzania (Tanzania Partner)**
World Vision Tanzania
S.L.P. 6070 Arusha, Tanzania
Barua Pepe ya Mawasiliano: david_ombeni@wvi.org
Simu: +255 687 231 757

## MWONGOZO kwa WAALIMU

Mwanzoni, masomo ya Wakati na Biblia yaliandaliwa ili yatumike kwa njia ya posta kukiwepo na kituo cha Shule ya Biblia kwa njia ya posta. Sasa hivi, masomo yanaendelea kutumika kwa wingi hata kwenye sehemu ambazo hazina ufanisi wa kutumia mfumo wa posta au hakuna kabisa mfumo wa posta hasa katika makanisa na shule zilizopo Afrika, India na maeneo mengine. Mwongozo wa kufundisha umeandaliwa kwa wale wanaotumia masomo ya Wakati na Biblia katika hali kama hizo. Mwongozo wa kufundisha katika kitabu hiki umeandaliwa kutumika kwa masomo ya daraja la tatu na la nne kwa watoto wenye umri wa wastani wa miaka 11-16 na zaidi.

Kila Mwongozo wa kufundisha hufuata vifungu vile vile vya Biblia vilivyopo katika somo la Wakati na Biblia. Masomo ya Wakati na Biblia na Mwongozo vimeandaliwa vitumike kwa kila wiki. Masomo ya mwezi Aprili yanahusu Pasaka na masomo ya mwezi Desemba yanahusu Krismasi.

Baadhi ya sehemu watakuwa wanatumia masomo yaliyo katika toleo la A4 la kila wiki na wengine watakuwa wanatumia kitabu cha A5 chenye masomo 24 ndani yake. Kwa kawaida, mwalimu au kiongozi hutoa somo la mwezi toleo la A4 na kila wiki sehemu ya kazi hujazwa kanisani au shuleni au hupelekwa nyumbani na kurejeshwa wiki inayofuatia. Mwishoni mwa mwezi, mwalimu au kiongozi hukusanya somo na kwenda kusahihisha kama inavyotakiwa na kumrudishia mwanafunzi/mtoto kazi iliyosahihishwa mapema iwezekanavyo.

Unapotumia kitabu, mwisho wa kila kipindi, vitabu hukusanywa na kusahihishwa. Tumegundua katika sehemu nyingi kuwa, hili haliwezekani. Hivyo basi, pale darasani masomo yanaweza kugawanywa kwa wanafunzi wengine na mwalimu au kiongozi ataongoza usahihishaji wa somo na wanafunzi watasahihisha masomo ya rafiki zao na kutoa maksi. Nyuma ya kitabu kuna sehemu kwa ajili ya kuweka maksi ya kila somo la mwezi na pia mahali pa maoni kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Pia kuna cheti ambacho mwanafunzi anaweza kupewa kinachoonesha asilimia ya alama ambazo mwanafunzi amepata kwa masomo ya miezi sita.

Tutashukuru kama tutapata mrejesho kuhusu matumizi ya Miongozo ya Waalimu na kwa ajili ya vitabu vya Wakati na Biblia na mrejesho huo utumwe kwa stephen.gillham@besweb.com.

## MAANDALIZI KWA WAALIMU

Hatupendi kutoa shinikizo na kutokuwapa waalimu fursa ya kufanya mambo kwa njia zao wenyewe kulingana na mawazo na mipango yao wenyewe. Haya ni mapendekezo yanayoweza kutumika kwenye utumiaji wa masomo ya Wakati na Biblia.

- **Elewa habari vizuri –** Waalimu wanapaswa kuelewa habari ya Biblia vizuri kwa kadri iwezekanavyo na vile vile somo la Wakati na Biblia linaloendana na habari hiyo ya Biblia. Ni jambo zuri kwa mwalimu kuKamilisha Somo la Wakati na Biblia kabla ya kipindi. Mwongozo wa kila somo unapaswa kutumiwa kwa umakini kama chombo cha kumsaidia mwalimu anapojiandaa kwa ajili ya somo.
- **Elewa funzo ambalo watoto wanastahili kupata au kujifunza –** Juu ya kila mpangilio wa somo utaona maneno ‘Tunajifunza kuwa’ ikifuatiwa na makusudio mawili ya kujifunza ambayo tunatumaini kwamba watoto watayaelewa baada ya kumsikiliza mwalimu akifundisha na kuKamilisha Somo la Wakati na Biblia. Kusudio la kwanza la kujifunza linahusu ufahamu wa habari na la pili linamtia moyo mtoto kufikiri juu ya ufahamu huo, kuutumia na kuuitikia. Makusudio haya ya kujifunza ni sentensi kamilifu na fupi ya mawazo au kweli kuu zinazofundishwa katika somo. Waalimu wanaweza kuzitumia kwa ajili ya tathimini zao binafsi za ufundishaji na mafunzo ambayo watoto wamepata.
- **Toa Utangulizi –** Kwa masomo yote, tunaanzia mahali ambapo watoto wapo katika uzoefu wao wa hali husika. Tumependekeza njia kadhaa ambazo zinaweza kutumika kufanya utangulizi wa habari ili kuwawezesha watoto kuhusika katika kujadili mwanzo wa habari.
- **Fundisha –** Tumetoa dondoo muhimu katika habari. Tunaamini kwamba waalimu hawatazinukuu wakati wanafundisha habari lakini watakuwa na uelewa mzuri wa habari na wataweza kuifundisha katika njia inayofurahisha na kusisimua. Mwalimu atahitaji watoto waelewe mafunzo muhimu kutoka kwenye habari na kuwasaidia kuuelewa mwitikio watakaoupata kutoka kwenye habari waliyojifunza. Kwa usahihi, tumejaribu kuweka pamoja baadhi ya maelezo kwa ajili ya kufundisha habari. Haya yameandikwa katika maandishi *YA MCHALAZO (Italics)*.
- **Jifunze –** Kuna Mstari muhimu ambao umewekwa katika kila habari. Katika baadhi ya maeneo, kuna Mistari muhimu miwili. Mstari huu ulioongezwa unaweza kuwa rahisi kwa watoto kujifunza. Tunatumaini kwamba, watoto watajifunza Mistari muhimu na watakumbushiwa mstari huo mara nyingi iwezekanavyo ili waanze kujenga ufahamu wa Mistari muhimu ya Biblia.

- **Kamilisha –** Katika mazingira ya shule, utatambua uwezo wa watoto kwenye kukamilisha kazi na kiasi cha usaidizi ambao wanauhitaji kutoka kwa mwalimu. Kwa baadhi yao, itahitajika mwalimu asome maandishi katika somo na watoto kufuatilia habari ambayo sasa watakuwa wanaielewa. Watoto wengine wanaweza kusoma maandishi ya somo peke yao. Kwa hali yoyote kati ya zilizotajwa, ni wazo zuri kuwahamasisha watoto wawe makini na kuwapa maelekezo muhimu yanayohusiana na maswali. Kama unatumia masomo ya Wakati na Biblia katika maeneo ambayo siyo shule, ni muhimu uwepo ili watoto wasichukulie masomo kama kazi isiyo na mvuto au kama mtihani. Masomo haya yanapaswa kuwa ya kufurahisha na kutia moyo. Ni muhimu kuwasifia watoto wanapoendelea kufanya masomo na kujibu maswali.
- **Kumbuka –** Tunashauri matumizi ya maswali mafupi na maigizo ili kuwasaidia watoto kujifunza na kurudia habari ili kuielewa vyema.
- **Kuonesha –** Tunatambua kuwa katika baadhi ya mazingira, sio rahisi kupata vielelezo au video. Lakini, ni muhimu kadri iwezekanavyo kuwa na picha au vitu vinavyoweza kuwasaidia watoto kuielewa habari vizuri zaidi. Vielelezo vitakuwa muhimu sana wakati ambapo mwalimu anaelezea habari. Kadri iwezekanavyo kwenye kila somo, tumetoa maelezo kuhusu picha kutoka kwa picha za www.freebibleimages.org (FBI) ambazo zinaweza kupakuliwa bure kwenye tovuti yao. Mwishoni mwa Mwongozo huu kuna viambatanisho vyenye viungo (hyperlinks) vya picha kadhaa kutoka kwenye tovuti ya Free Bible Images ambazo zinafaa kila habari ya Biblia.
  Kama kuna kinakilishi (photocopier), baadhi ya picha za Bibletime zinaweza kufanywa kuwa kubwa, kupakwa rangi na kutumiwa kufundisha.

## Kupangilia Muda

- **Ratiba –** Tumeweka ratiba sawa kwenye mwongozo wa kufundisha kila somo lakini mwalimu anaruhusiwa kubadilisha ratiba hii mara kwa mara kulingana na mahitaji ya darasa lake/ watoto anaowafundisha.
  1. Utangulizi na kuwaambia watoto habari husika – Takriban dakika 15
  2. Kufundisha Mstari muhimu – dakika 5 hadi 10
  3. Kujaza nakala ya somo – dakika 20
  4. Maswali na shughuli zinginezo- dakika 5 hadi 10

Kumbuka msemo muhimu:

“Niambie na nitasahau,
Nioneshe na nitakumbuka,
Nihusishe na nitaelewa”

## Mtaala wa Wakati na Biblia

| | Daraja 0<br>(Chekechea/ Kabla ya Kuanza Shule)<br>Daraja la Kwanza<br>(Miaka mitano hadi saba)<br>Daraja la Pili<br>(Miaka nane hadi kumi) | Daraja la Tatu<br>(Miaka kumi na mmoja hadi kumi na mitatu) | Daraja la Nne<br>(Miaka kumi na minne na zaidi) |
|---|---|---|---|
| SOMO LA KUANZIA | Somo la kuanzia – Utangulizi | Somo la kuanzia – Utangulizi | Somo la kuanzia – Utangulizi |
| MFULULIZO WA A | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Ibrahimu<br>6. Ibrahimu<br>7. Petro<br>8. Petro<br>9. Yakobo<br>10. Wakristo wa Kwanza<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maombi<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo na Kuanguka<br>2. Matukio ya Kwanza-Mwanzo<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maisha ya Ukristo<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA B | 1. Maisha ya kwanza ya Kristo<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Mifano<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Walioandika vitabu vya Injili<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yakobo na familia yake<br>7. Yusufu<br>8. Matendo ya Mitume 2: 42 – Njia iliyoko mbele<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Amri<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA C | 1. Danieli<br>2. Miujiza zaidi<br>3. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu na Samweli<br>6. Daudi<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Yona<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>3. Miujiza zaidi<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8 Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu ambao Mungu aliwatumia – Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Maneno ya Kristo<br>3. Nguvu za Bwana<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu zaidi wa Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi |

| | **B1 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Kwanza – Mifano**<br>**Mada – Jirani yangu ni nani?** | **B1 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Kwanza – Mifano**<br>**Mada – Wadeni wawili.** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 10: 25-37***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 10: 27***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Jirani zetu ni wale ambao wanahitaji msaada wetu bila kujali rangi au dini zao<br>2. Tunapompenda Mungu tunaweza kuonesha upendo wetu kwa kuwasaidia jirani zetu katika mahitaji yao ya kiroho, kimwili ama vitu. | **Neno la Biblia:** ***Luka 7: 36-50***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Warumi 5:*** 1<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Sisi sote ni wadeni machoni mwa Bwana Yesu Kristo - sote tumetenda dhambi. Kwa hiyo tu wadeni kwa Mungu.<br>2. Ikiwa kama tumekwisha kusamehewa dhambi zetu tunapaswa kuishi kwa upendo na kujitoa kwetu kwa Bwana Yesu Kristo iwe ni alama ya maisha yetu katika utakatifu na utumishi wetu. |
| **TOA UTANGULIZI** | Jadili nini maana ya jirani na tengeneza wazo kuwa si ukaribu ambao unatufanya sisi kuwa majirani wazuri bali ni ule wema na urafiki tunaouonesha kwa yeyote anayehitaji msaada wetu. | Toa taarifa za msingi za mfano huu kwa kuonesha kuwa ina:<br>● Watu watatu halisia – Bwana Yesu, mwanamke mwenye dhambi na Simoni Farisayo;<br>● Watu watatu dhahania – Mkopeshaji, mtu aliyewiwa dinari 500 na mtu aliyewiwa dinari 50;<br>● Maswali matatu – ***mstari wa 42, 44 & 49***. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. a) Mtu aliyeangukia kati ya wanyang'anyi ***(mstari wa 30)*** alipigwa, akajeruhiwa na kuachwa karibu na kufa.<br>b) Kuhani na Mlawi wakampita.<br>c) Msamaria akamhurumia ***(mstari wa 33)*** akamfunga majeraha yake akamchukua mpaka nyumba ya kulala wageni na kuhakikisha anahudumiwa mpaka atakaporudi kutoka alikokuwa anaenda. ***(mstari wa 33-35)***<br>2. a) Kutokana na mwanadamu kutokutii ndani ya bustani ya Edeni, Mungu hutuona sisi kama wafu katika dhambi. ***(Waefeso 2: 1)***<br>b) Mungu alituhurumia sisi kama wenye dhambi na alimtuma mwanae Yesu Kristo katika ulimwengu huu ili kwamba kupitia kifo na kufufuka kwake tupate kuponywa kutoka katika dhambi na madhara yake katika maisha yetu. Kama msamaria mwema, Yesu alikuja pale tulipokuwa ni wahitaji.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Jirani yangu ni nani? | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Kujihesabia haki kwa Simoni; machozi ya mwanamke ya toba, furaha, upendo na shukrani; na Bwana Yesu aliyeweza kusoma mawazo ya Simoni pale alipofikiria Yesu amuepuke mwanamke huyu mwenye dhambi. ***(mstari wa 36-39)***<br>2. Mfano huu unakusudiwa kuonesha kuwa Bwana Yesu ni mkopeshaji kwetu. Sisi sote tu wadeni wa Mungu na Yesu alipokufa msalabani, alitulipia deni! Yesu alijua kuwa Simoni alijiona kama mdaiwa wa dinari 50 na yule mwanamke kama mdaiwa wa dinari 500. Yesu alikusudia Simoni ajifunze kuwa hakuna viwango katika dhambi. Aliyewiwa dinari 500 na aliyewiwa dinari 50 hawakuweza kulipa madeni yao lakini mkopeshaji aliwasamehe wote. ***(mstari wa 40-43)***<br>3. Alipoulizwa ni mdaiwa yupi ambaye angempenda mkopeshaji zaidi. Ilibidi Simoni akiri kuwa; ni yule aliyesamehewa zaidi. ***(mstari wa 42)*** Yesu aligeuza mtazamo aliokuwa nao Simoni kwa yule mwanamke aliyeonesha upendo kwa Yesu, ukilinganisha na kukosekana kwa upendo na heshima kwa Simoni. ***(mstari wa 44)*** Yesu pia anaonyesha kwamba Yeye anaweza kusamehe dhambi lakini ilikuwa ni imani ya yule mwanamke iliyomwokoa na siyo kile ambacho alikifanya. ***(mstari wa 48-50)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Wadeni wawili. |
| **REJELEA SOMO** | Waulize kila mmoja kuhakikisha kuwa, anayafahamu matumizi ya mfano huu. Kumpenda Mungu ni kitu bora zaidi tunachoweza kukifanya katika maisha yetu, na tunaonesha upendo kwa Mungu kwa kupendana sisi kwa sisi bila kujali ni nani anahitaji upendo wetu. | Soma ***Matendo 13: 38-39*** na jadili namna maandiko haya yanavyojumuisha kwa ufupi kitu ambacho Bwana Yesu alikuwa akikifundisha katika somo hili. Soma ***Waefeso 4: 32*** na jadili namna ambavyo wale waliosamehewa dhambi wanatakiwa wawatendee wengine, na wanavyojisikia baada ya kusamehewa na Mungu dhambi zao zote (madeni yote) |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je wanafunzi wameokoka na kubadilika?<br>2. Kama ndiyo, fikiria njia ambazo wanaweza kuwa majirani wema, au marafiki wema kwa watu wafuatao:<br>a) Mtu ambaye hajaokoka (kiroho).<br>b) Mtu mwenye ulemavu (kimwili).<br>c) Watu ambao hawana chakula cha kutosha upande fulani wa dunia (vitu). | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Simoni alimhudumia Bwana Yesu kwa kumshutumu kwamba hakustahili kuchangamana na wenye dhambi na hakuna ushahidi kabisa kuwa alitubu kwa fikra zake dhidi ya yule mwanamke ili kupata msamaha na amani. ***(mstari wa 50)***<br>2. Jadili nao kuhusu mitazamo yao kwa Bwana Yesu na waulize wanafunzi kama wamekwishakutubu dhambi zao na kumwendea Bwana Yesu kwa ajili ya msamaha?<br>3. Ikiwa wamekwisha kusamehewa, Je wanampa Bwana Yesu muda wao wa thamani, karama ama mali zao? Jadili namna mwanamke alivyoitikia. |

| | B1 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Pili – Mifano<br>Mada – Mkulima tajiri | B1 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Pili – Mifano<br>Mada – Jirani yangu ni nani? |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 12: 13-21***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 12: 15***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mkulima Tajiri alikuwa tajiri mwenye mali lakini alikuwa amefilisika kiroho, kwa sababu alimwacha Mungu nje ya maishani yake.<br>2. Kama tunamweka Mungu mbele na siyo kutanguliza vitu kwanza katika maisha yetu, tutatumia maisha yetu kwa utukufu wake ikiwa tuna vitu vingi ama vichache. | **Neno la Biblia:** ***Luka 10: 25-37 pia Wafilipi 2: 1-11***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 10: 27***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mtu anayetuhitaji sisi, bila ya kujali rangi ama dini yake, ni jirani yetu. Ni jukumu letu kumuonyesha wema.<br>2. Kupitia kifo chake msalabani, Bwana Yesu anaweza kutuokoa sisi kama vile alivyofanya kwa Msamaria. Anaweza kutuweka sisi mahali salama na kutupa mahitaji yetu. Tazama pia Daraja la Tatu Somo la Kwanza. |
| TOA UTANGULIZI | Ongelea kuhusu mali zinazotamaniwa.<br>Jadili kuhusu dhambi ya kutamani vitu na hakikisha wanaelewa kuwa ni uchoyo kumiliki na kujilimbikizia vitu vya duniani ambavyo hatutavichukua tutakapokufa.<br>Rejea Amri Kumi na elezea kwa nini ile ya mwisho inasema “Usitamani”. ***(Kutoka 20: 17)*** | Ongelea kuhusu jirani zetu ni akina nani?<br>Jadili na wanafunzi kuwa ujirani ni kuwa mtu mwema na rafiki kwa wale wote wenye mahitaji na kuwa na ‘ukaribu’ nao. Yesu anategemea watoto wake kuwa wema kwa wote ukijumuisha na wale ambao hawatupendi sisi kwa kuwa sisi ni Wakristo. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yesu alimwita mtu huyu “mpumbavu” kwa kuonesha upungufu wake wa ufahamu kuhusu umuhimu wa mambo ya kiroho na vitu vya asili ambavyo ni vya muda.<br>2. Alikuwa mpumbavu katika njia zifuatazo:<br>a) Mpumbavu asiye na Mungu aliishi maisha yake bila Mungu. Maisha yanaweza kuwa yamejaa “kila kitu” lakini ikiwa hayana Mungu ni bure. Kijana hakufahamu kwamba mali zake zote zilitoka kwa Mungu.<br>b) Maskini mpumbavu – Hakika alikuwa tajiri maskini. Yaani alikuwa maskini kwenye maisha yake ya milele. Aliweka moyo wake kwenye utajiri kuliko kwa Mungu.<br>c) Mpumbavu mwenye ubinafsi. Kwenye ***mstari wa 17-19***, utagundua silabi **“ni”** imetajwa mara 6, **“angu”** mara 5 na **“nita”** mara 4. Mungu aliyempa utajiri alikuwa hayumo kwenye mawazo yake. Alidiriki hata kuiita nafsi yake – ee nafsi yangu.<br>d) Mpumbavu mwenye bidii – Alikuwa na ubinafsi kwenye juhudi zake kwa kuwa alitamka juu ya usalama wake kwa miaka mingi ijayo, asiyependa shida na alijiburudisha nafsi yake kwa kula na kunywa. ***(mstari wa 19)***<br>e) Mpumbavu aliyepotea – Mungu ambaye mpumbavu huyu alikuwa amemsahau, “aliitaka roho ya mtu huyu” ***(mstari wa 20)*** Mungu ndiye anayetupa maisha mapya na anaweza kuyatwaa.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Mkulima tajiri. | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mwana sheria aliyebobea katika sheria za Musa alipomuuliza Yesu afanye nini ili aurithi uzima wa milele, Yesu alimwelekeza kwenye Torati na akamwambia ilitaka nini. Ilihitaji upendo wote kwa Mungu na kwa jirani yake. Yesu alikuwa akimwonesha kusudi la Torati au Amri kumi kuwa haikuwa kwa ajili ya kutukomboa kutoka dhambini bali ilikuwa ni kutuonesha jinsi gani sisi wanadamu tu wenye dhambi. ***(10: 26-28)***<br>2. Mwana sheria alipofahamu kwamba amepungukiwa na hajakidhi viwango vya Mungu, alitakiwa kumwomba Bwana amwokoe. Lakini katika kiburi na kujivuna kwake alimuuliza Bwana ‘Jirani yangu ni nani?’ Ili kumjibu, Bwana anawaambia habari ya Msamaria mwema. Kuhani na Mlawi walikuwa ni Wayahudi na Wayahudi waliwachukia sana Wasamaria. Walikataa kuwasaidia lakini katika habari hii, Msamaria aliyedharauliwa alifika akamwokoa yule majeruhi. Mwana sheria alilazimika kukubali kwamba Msamaria alidhihirisha kuwa ni jirani wa kweli kwa yule Myahudi aliyejeruhiwa. ***(10: 29-37)***<br>3. Tunauona udhaifu wa Kuhani na Mlawi na Udhaifu wa sheria katika kuwasaidia wenye dhambi na Msamaria mwema anatukumbusha jinsi Bwana Yesu alivyokuja tulipokuwa dhaifu, akatuokoa kutoka kwenye adhabu ya dhambi zetu.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Jirani yangu ni nani? |
| REJELEA SOMO | Mkulima tajiri alifanya makosa makubwa matatu:<br>1. Hakutambua kusudi la maisha. *Soma **Wafilipi 1: 21** na elezea kusudi la maisha ya Paulo.*<br>2. Aliutumia utajiri wake kwa ajili yake mwenyewe. *Soma **Wafilipi 4: 19** na elezea jinsi Mungu anavyoshughulika na mahitaji yetu pale tunaposhughulika na mahitaji ya watu wengine.*<br>3. Alikuwa na hofu ya kesho na alipoteza nafsi yake. *Soma **Marko 8: 36-37** na jadili jinsi maandiko haya yanavyohusiana na mkulima tajiri.* | Rejea katika somo la Biblia kitabu cha Wafilipi na andika kwa ufupi somo hili kwa kuonesha kuwa, ***mistari ya 1-4*** inaonesha thamani ya ujirani kwa Wakristo na ***mistari 5-11*** inaonesha jinsi Bwana Yesu alivyo mfano dhahiri wa upendo kwa kuwa alikufa kwa ajili ya wengi. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Tengeneza orodha ya njia ambazo tunaweza kutumia mali zetu kwa kuwasaidia watu wengine. Tafuta tofauti kati ya “shauku” na “ uhitaji ”<br>2. Fikiria kwamba wale wasio wakristo wafanye jambo hili kuwa kipaumbele yaani kuweka imani yao kwa Kristo Yesu ***(Yohana 3: 16)*** na wamweke Yeye awe wa kwanza kwenye maisha yao. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Kila mtu ni jirani yetu:<br>1. Tunawezaje kuwasaidia wale ambao wana mahitaji ya kimwili, kiroho na mahitaji ya vitu?<br>2. ***Luka 6: 35*** inasema nini kuhusu jirani mwema? Je namna gani tunaweza kulitendea kazi jambo hili? |

| | B1 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Tatu – Mifano<br>Mada – Mpanzi | B1 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Tatu – Mifano<br>Mada – Mtu mpumbavu |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Marko 4: 1-20***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Marko 4: 20***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mbegu ni neno la Mungu.<br>2. Aina za udongo inawakilisha mioyo ya wanadamu na jinsi inavyopokea neno la Mungu. | **Neno la Biblia:** ***Luka 12: 13-21***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 12: 15***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Kuwa na tamaa ni dhambi kwa kuwa maisha ya mtu hayatokani na wingi wa mali tulizo nazo.<br>2. Kujielekeza kwenye kujilimbikizia mali kwa kupoteza nafsi ya mtu, ni upumbavu wenye matokeo yenye madhara. Tazama pia Daraja la tatu Somo la pili. |
| **TOA UTANGULIZI** | Elezea kwamba kila mara Yesu alisema kwa mifano kusisitiza baadhi ya kweli alizokuwa akifundisha. Kwa ujumla mifano ilikuwa ina maana ya ndani ya kiroho. Wakati mwingine hakuelezea maana lakini zamu hii alitoa maelezo na ufafanuzi kwa kina.<br>Mahali tofauti ambapo mbegu zilipandwa ziliwakilisha miitikio tofauti ya watu baada ya kulisikia neno la Mungu. | Jadili historia ya mfano huu. Mtu aliyemwomba Yesu aingilie kati mgogoro uliokuwepo juu ya urithi baina yake na nduguye. Wakumbushe wanafunzi jinsi Yesu alivyomuonesha mtu huyu kwamba lengo la ujio wake Ulimwenguni lilikuwa ni kuwaokoa waume kwa wake wenye dhambi na siyo kusuluhisha migogoro ya mirathi. Haya ni mambo madogo ukilinganisha na umuhimu wa mambo ya kiroho ambayo yanahitaji umakini wetu. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Udongo ulio njiani ***(mstari wa 15)*** ni yule asemaye “HAPANA” kwa Bwana Yesu. Shetani anatazamwa kama ndege anayenyakua neno la Mungu. Mtu huyu anakuwa hajabadilishwa na neno la Mungu.<br>2. Udongo wa kwenye mwamba ***(mstari wa 16-17)*** ni mfano wa mtu yule ambaye anaikiri imani, anatembea vizuri kwa muda fulani na panapotokea udhia anatakiwa kusimama kwa Kristo, yeye huona kuwa gharama ni kubwa na kuamua kuacha mambo yote. Pale panapotokea udhia ukiri wake usio na uhalisia huonekana dhahiri.<br>3. Udongo wa kwenye miiba ***(mstari wa 18-19)*** ni wale ambao huanza vizuri na huonekana kuwa ni wakristo halisi. Baadaye kwakuwa wameshikwa na shughuli na mali na vitu vya duniani huacha madai ya kuwa ni wakristo; ndio wale wasiozaa “matunda “.<br>4. Udongo mzuri ***(mstari wa 20)*** ni watu wale walipokeao neno – wakatubu dhambi zao na wakaweka tumaini lao kwa Bwana Yesu Kristo – na kumfuata Yeye kwa uaminifu na kwa gharama zote.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Mpanzi. | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mfano huu unaonesha kuwa mali zetu sio msingi wa maisha. Tumepewa na Mungu na tumekusudiwa kuzitumia kwa utukufu na heshima ya Mungu. Mtu huyu alipaswa kuelewa kwamba alipaswa kuwagawia wahitaji mali zake.<br>2. Ana mipango yake ya wakati ujao – tazama maisha yake ya kutomtegemea Mungu anapotumia maneno kama 'mimi' na 'yangu' katika ***mistari 17-19***. Mungu alikuwa na mipango mingine kwa ajili ya maisha ya mtu huyu na alimwambia angekufa usiku ule ***(mstari wa 20)***. Mipangilio yake ingeishia kaburini na alikuwa mpumbavu kwa kuwa hakufanya maandalizi kwa ajili ya uzima wa milele – Tazama maonyo katika ***Amos 4:12***.<br>3. Onesha jinsi Mungu anavyouliza swali kwa dhati kabisa katika habari hii ‘Na vitu ulivyojiwekea tayari vitakuwa vya nani?’ ***(mstari wa 20)***<br>4. Onesha kuwa tunapaswa kutumia karama na vipaji vyetu ili kuuendeleza ufalme wa Mungu.<br><br>**Elezea mstari muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Mtu mpumbavu. |
| **REJELEA SOMO** | Hakikisha kuwa wanafunzi wanaelewa utofauti wa aina nne za udongo. Katika majadiliano ongelea juu ya viwango tofauti vya “kuzaa matunda” katika ***mstari wa 20***; thelathini, sitini na mia moja na uoneshe kwamba, maisha yenye matokeo bora zaidi ni ya wale ambao kwa hiari yao wenyewe hulitii neno la Mungu na kuona fahari katika kufanya hivyo. | Fikiria jinsi ***Mithali 11: 4 & 29*** na ***Mathayo 6: 19-21*** zinavyotoa muhtasari mzuri wa somo hili. Pia angalia ***Kutoka 20: 17*** kuhusiana na tamaa ya vitu. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Ni aina ipi ya udongo inawakilisha vizuri kila moyo ulivyo?<br>2. Kwa wakristo, kuna uzoefu gani kwa mtu anayesimama kwa Kristo Yesu shuleni ama popote pale?<br>3. Kama mkristo, fikiria njia kadhaa ambazo maisha yanaweza kumzalia Kristo matunda. Je sote tulenge kiasi kipi? thelathini,sitini ama mia moja?<br>4. Usomaji wa Biblia kila siku, kukariri mistari muhimu na kuomba huwasaidia wakristo kuweka mioyo yao kwa Mungu na kuwa wenye matunda katika maisha yao. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1 Umuhimu wa kuhakikisha kuwa, kusudi la kweli la maisha ya mtu ni ‘kwangu mimi kuishi ni Kristo”. (Paulo katika ***Wafilipi 1: 21***)<br>2 Umuhimu wa kutumia mali zetu kwa faida ya wengine. Tengeneza orodha ya fikra za kuwasaidia wengine.<br>3 Umuhimu wa kutokufuata tamaa zinazoleta madhara katika wokovu wetu. |

| | B1 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Mifano<br>Mada – Kuwasamehe wengine | B1 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Mifano<br>Mada – Karamu kubwa |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mathayo 18: 21-35***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Waefeso 4: 32***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mfano huu ulifafanuliwa kuwafundisha wakristo namna ya kusamehe.<br>2. Tusiwe na ukomo wa msamaha kwa wengine.. | **Neno la Biblia:** ***Luka 14: 15-24***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 6: 37***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu ameahidi karamu mbinguni kwa wale wanaoitikia mwaliko wake 'njooni kwangu'. ***(Mathayo 11: 28)***<br>2. Miongoni mwetu tuliomjia Bwana Yesu kwa ajili ya wokovu tuna wajibu wa kuwashawishi wengine kumwitikia Yesu. |
| TOA UTANGULIZI | Elezea tatizo alilokuwa nalo Petro kuhusu msamaha. ***(18: 21)*** Elezea kwamba alifahamu kuwa katika Agano la Kale mtu alisamehewa walau mara tatu au mara nne ***(Amosi 2: 6)***. Kama mwanafunzi wa Yesu Kristo, Petro anajisikia kuwa mkarimu zaidi ambapo anapendekeza kusamehe mara saba ***(mstari wa 21)***. Hata hivyo, Bwana anasema "sabini mara saba" ambapo kiuhalisia ina maana tusiwe na ukomo wa msamaha wetu kwa wengine. | Onesha jinsi kule Mashariki watu wenye vyeo wanavyoweza kutoa mialiko ya aina mbili kwenye karamu iliyopangwa. Mwaliko wa kwanza ulionesha kuwa maandalizi yalihitajika na mwaliko wa pili ulionesha kuwa karamu ilikuwa tayari. Katika hili waalikwa wote hawakuwa na sababu ya kukataa ama kutoa udhuru. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Bwana wa yule mtumwa alipogundua kuwa mdeni wake alikuwa hana uwezo wa kulipa deni lake kubwa, alimwonea huruma na akamsamehe lile deni. ***(mstari 25-27)*** Hiki kilikuwa ni kitendo cha rehema, kumuondolea adhabu aliyostahili mtumwa yule.<br>2. Kama wenye dhambi, hatuwezi kulipa deni letu kubwa la dhambi na tunahitaji rehema za Mungu ili kuepuka adhabu yake. Tunaweza kupata wokovu kupitia kazi ya Kristo aliyelipa deni la dhambi ya ulimwengu msalabani. Mungu alimtoa Mwanawe "ambaye alitoa nafsi yake iwe fidia ya wengi" ***(Mathayo 20: 28)***<br>3. Mtumwa aliyesamehewa angelimsamehe mtumwa mwenzake aliyemdai kiasi kidogo sana (takribani Tsh 15,000) ukilinganisha na kiwango ambacho yeye mwenyewe aliwiwa (takribani Tsh bilioni 3). Alisahau rehema aliyooneshwa.<br>4. Tunapaswa kuwatendea wengine kama vile Bwana Yesu alivyotutendea sisi.Tukisema sisi ni wake na ni mali yake, ni lazima tuwasamehe wengine, ikiwa ni pamoja na maadui zetu. ***(Angalia Mstari Muhimu)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kuwasamehe wengine. | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Karamu hii kuu inatukumbusha sisi ukweli kwamba Bwana Yesu alimaliza kazi ya wokovu kwa kufa msalabani na matokeo yake mwaliko wa Injili unawafikia wote.<br>2. Sababu tatu za kutoa udhuru hazikuwa za msingi kwa kuwa katika kila sababu, mipango ingeweza kufanywa ili kuweza kuhudhuria: Sababu ya kwanza ***(mstari wa 18)***; licha ya kuomba radhi ni vigumu kuamini Myahudi anaweza kununua ardhi bila kuiona na kwa vile karamu ilikuwa jioni asingeweza kuiona hata hivyo. Sababu ya pili ***(mstari wa 19)***; Huyu mtu ni mkaidi sana, haombi radhi na anawaza ng'ombe wake kwanza. Sababu ya tatu ***(mstari wa 20)***; Mtu huyu alitoa sababu dhaifu lakini angeliweza kumleta mkewe kwenye karamu kama asingelikuwa mbinafsi.<br>3. Sababu hii ya kwanza inawakilisha wale ambao wanaweka kipaumbele kwenye mali zao, sababu ya pili ni wale ambao wametingwa sana na shughuli zao na sababu ya tatu inawakilisha wale ambao wanatumia muda wao mwingi kwa majukumu ya nyumbani.<br>4. Mwenyeji hafurahishwi na anahisi kudharauliwa kwa sababu ya hizi sababu zilizotolewa na anamtuma mtumwa wake kwenda 'barabarani na mipakani' kuwaalika maskini, viwete na vipofu. ***(mstari 21 & 23)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Karamu kubwa. |
| REJELEA SOMO | Jadili jinsi kifungu hiki kinavyoonesha 'rehema' na 'neema'. Somo la ***Tito 3:5***. 'Si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi, bali kwa rehema yake alituokoa', na ueleze kwamba rehema hutoa njia ya haki ambayo kwayo tunaweza kuepuka adhabu ya Mungu. Soma ***Waefeso 2:8*** 'Kwa maana mmeokolewa kwa neema.' Kuokolewa ni zawadi ya Mungu kwa neema – kutupa usalama wa milele ambao hatukustahili na hatuwezi kuulipia. | Eleza jinsi matumizi ya msingi ya mfano huu yanavyomaanisha kwamba wale walioikataa Injili walikuwa Wayahudi na kisha ikatolewa kwa mataifa ambao waliitikia zaidi.<br>Hakikisha wanafunzi wanaelewa umuhimu wake kwao kwa kuwa wale wanaoendelea kukataa rehema na neema ya Bwana watajikuta kwamba siku moja wamechelewa na milango ya karamu ya injili Mbinguni imefungwa.<br>Fikiria baadhi ya udhuru ambao watu wanaweza kutoa leo wanapopinga Injili ya Yesu Kristo. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Namna gani somo hili linakupa changamoto juu ya "msamaha'?<br>2. Ikiwa kama tumesamehewa na Bwana Yesu, Kwa nini na sisi tusiwasamehe wengine?<br>3. Rejea ***Waefeso 4:32*** ili kupata sifa zingine tunazopaswa kuwa nazo ikiwa ni pmoja na 'msamaha.' | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Hakuna aliye mbaya sana kiasi cha kushindwa kuketi mezani pa mfalme kama ilivyooneshwa na wale waliotoka 'barabarani na mipakani'.<br>2. Ushawishi wenye upendo utumike katika kuwaleta watu wengine kwenye baraka ya wokovu. Bado kuna nafasi kwa watu kuingia kwenye ufalme wa Mungu. |

| | B2 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Kwanza – Miujiza<br>Mada – Maji kuwa Divai | B2 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Kwanza – Miujiza<br>Mada – Maji kuwa Divai |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Yohana 2: 1-11***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 2: 11***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Bwana Yesu ndiye tunayepaswa kumtii.<br>2. Tunapomwamini Bwana Yesu, huleta furaha katika maisha yetu. | **Neno la Biblia:** ***Yohana 2: 1-11***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 15: 14, Yohana 2: 5***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Kama tunampenda Bwana Yesu, tunapaswa kuyazingatia maelekezo ya Mariamu kwa watumishi huko kwenye harusi “Lolote atakalowaambia, fanyeni”. ***(Yohana 2: 5)***<br>2. Katika kuufanya muujiza huu, Bwana Yesu alikuwa akiudhihirishia umma ule kwamba hakika Yeye alikuwa ni Mungu katika umbo la mwanadamu, pamoja na kuimarisha imani ya wanafunzi waliomwamini. |
| **TOA UTANGULIZI** | Wadokeze kuhusu harusi za Mashariki.<br>Elezea kwamba katika kifungu hiki, Mariamu anatajwa kama “mama wa Yesu” katika ***mstari wa 1***. Elezea kwamba Bwana Yesu hakuwa mashuhuri kwa kuwa alikuwa mwana wa Bikira Mariamu lakini Mariamu alifahamika vizuri kwa kuwa alikuwa ni mama wa Bwana. Onesha kwamba mara zote Biblia imempa nafasi ya juu Bwana Yesu na siyo Mariamu. | Jadili miujiza ni nini, na ni kwa nini imeandikwa kwenye Injili zote.<br>Injili ya Yohana imeandika takribani miujiza saba, yote ilifanyika hadharani ambapo muujiza wa Kana ya Galilaya ni wa kwanza. Wanafunzi wanaweza kuambiwa watafute baadhi ya miujiza mingine.<br>Pia wadokeze kuhusu harusi za Mashariki. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Uamuzi wa kumwalika Bwana Yesu kwenye harusi ulikuwa ni wa hekima sana, ni sawa na uamuzi wa kumualika Yeye ndani ya mioyo yetu, majumbani mwetu, maisha yetu ya kawaida ama maisha yetu ya shuleni ulivyo wa busara sana<br>2. Wageni walivunjika moyo pale walipotindikiwa divai mwanzo kabisa wa harusi, lakini katika hali ile walimtazama Bwana Yesu kwa msaada. ***(2: 4 & 5)***<br>3. Divai njema ilitumika mpaka mwisho ikitukumbusha maisha ya mkristo yanavyokuwa mazuri nyakati zote.<br>4. Muujiza huu ulimdhihirisha Kristo kama mwana wa Mungu na zaidi uliimarisha imani ya wanafunzi wake. ***(2: 11)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Maji kuwa divai. | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Bwana Yesu, mama yake na wanafunzi wote wa Yesu walikuwa ni wageni kwenye harusi ambapo maji yaligeuzwa kuwa divai<br>2. Mariamu aliwaelekeza wale watumishi kwa Bwana Yesu na katika maneno yake ya mwisho ananukuliwa akiwaambia wale watumishi kuwa, “lolote atakalowaambia fanyeni” akiwaelekeza kuwa Bwana Yesu ndiye wanayepaswa kumtii kuliko mtu mwingine awaye yote. ***(2: 4 - 5)***<br>3. Divai njema ilitumika mpaka mwisho ikitukumbusha maisha ya Mkristo yanavyokuwa mazuri nyakati zote.<br>4. Muujiza huu ulimdhihirisha Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu na zaidi uliijenga imani ya wanafunzi. ***(2: 11)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Maji kuwa divai. |
| **REJELEA SOMO** | Rejea muujiza huu kupitia maswali yenye kuwasaidia wanafunzi kujibu katika Daraja la tatu, B2, Somo la kwanza. | Rejea somo kwa matumizi ya kila pointi hapo juu kwenye maisha ya mkristo. Angalizo:-<br>1. Divai katika Biblia huzungumzia furaha. Pale Mariamu aliposema “Hawana divai” ***(mstari wa 3)***, alikuwa akiwaelezea wale ambao hawajamwamini Bwana Yesu, kwa kuwa wasioamini hawana furaha ya kudumu.<br>2. Wale wanaompenda Bwana Yesu hutenda yale anayosema katika neno lake yaani Biblia.<br>3. Yesu anadhihirishwa waziwazi kama Mwana wa Mungu. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Jadili ni nini maana ya kumwalika Bwana Yesu ndani ya mioyo yetu? Soma ***Mithali 3: 5-6*** ili kubaini namna gani Bwana atatusaidia kuishi maisha yenye faida ndani yake.<br>2. Soma ***Zaburi 16: 11*** ili kubaini furaha iwangojeao wale wote wanaomjua Bwana Yesu kama Mwokozi wa maisha yao watakapofika Mbinguni. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Fikiria jinsi tunavyomwamini Bwana Yesu kama Mwokozi wa maisha yetu.<br>2. Jadili umuhimu wa kusoma Biblia na kuomba mara kwa mara kujua mapenzi ya Bwana wetu kwenye maisha yetu. |

| | B2 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Pili – Miujiza<br>Mada – Kuponywa kwa kijana | B2 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Pili – Miujiza<br>Mada – Kuponywa kwa kijana |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Yohana 4: 43-54***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***John 4: 50***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Kijana wa diwani alikuwa ni mgojwa sana kiasi cha kufa, na aliponywa na Yesu licha ya umbali uliokuwepo baina yao.<br>2. Sote tunazaliwa wenye dhambi tukiwa mbali na Bwana Yesu kwa jinsi dhambi zetu zinavyotutenga naye, lakini tunapotubu na kumrudia Yeye kwa ajili ya msamaha, anaweza kutupa maisha mapya. | **Neno la Biblia:** ***Yohana 4: 43-54***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 16: 31; Warumi 10: 9***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Kijana wa diwani alikuwa karibu na kifo cha kimwili na Yesu pekee ndiye aliyekuwa na uweza wa kumfanya kuwa hai tena.<br>2. Katika mtazamo wa kiroho, dhambi yetu ni ugonjwa ambao utasababisha kifo cha kiroho na ni Bwana Yesu pekee ndiye anaweza kutupa uzima wa milele. |
| **TOA UTANGULIZI** | Wakumbushe wanafunzi kuwa Bwana Yesu kwenye safari yake ya kwanza kule Kana, aligeuza maji kuwa divai na watu waliendelea kuona muujiza mwingine mkubwa uliofanyika huko – uponyaji wa kijana wa diwani.<br><br>Tumia ramani kwenye somo kuonesha kwamba ingawa Yesu alikuwa Kana, kijana alikuwa Kapernaumu lakini uweza wa Yesu ulimfikia kule kule aliko licha ya kutokuwa pamoja naye mahali pale. | Wakumbushe wanafunzi kwamba Bwana Yesu alitenda muujiza wake wa kwanza kule Kana na umaarufu wake ulisambaa sana kiasi kwamba baba wa yule kijana ambaye ni ofisa kwenye kasri la Herode alimsihi amponye mwanaye. Yule diwani alidhani Bwana Yesu angelisimama karibu na kijana ili amponye.<br>Bwana Yesu hakumkemea kwa kutokuwa na imani bali alimtendea kwa kile kiwango cha imani alichoonesha na kumpa zaidi.<br>Onesha kwamba Bwana Yesu alikuwa hapendezwi na imani iliyokuwa imejengwa katika miujiza ila iliyokuwa imejengwa kwenye neno lake pekee – amini kwanza kisha uone! |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Baba wa kijana huyu alikuwa ni myahudi na afisa wa mfalme Herode. Anaonekana kuwa alikuwa na imani kubwa kwa Bwana Yesu kuliko Wayahudi wenzake na alimsihi Bwana aje amponye mwanawe kwa kuwa alikuwa ni mgonjwa sana ***(4: 47)***<br>2. Baba wa kijana yule alidhani kuwa Bwana Yesu angehitajika kusimama karibu na kijana ili amponye lakini Bwana alimjibu kuwa kijana wake alikuwa amekwisha kupona na diwani aliamini maneno ya Bwana naye akashika njia kurudi nyumbani ***(4: 50)***<br>3. Alipowauliza watumwa wake ni muda gani kijana alikuwa amepona, majibu yao yalimhakikishia kwamba ilikuwa ni muda ule ule ambapo Bwana Yesu alimwambia kijana yu mzima. ***(4: 52-53)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kuponywa kwa kijana | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. **Kijana mgonjwa na maombi ya baba yake.** Ugonjwa na mauti hutujia sote, utajiri au umaskini, lakini wote tunamhitaji Bwana Yesu kukutana na mahitaji yetu ya kiroho. Bwana Yesu hufananisha dhambi na ugonjwa – rejea ***Mathayo 9: 12-13***. Biblia hutufundisha pia kwamba wale wote wanaomjua Bwana Yesu wana uzima wa milele na wale wasiomjua Yeye hawana huo uzima wa milele ***(1 John 5: 10-14)***<br>2. **Majibu ya Yesu.** Bwana Yesu alikuwa akiijaribu imani ya yule diwani pale alipomwambia, “enenda mwanao yu hai”' ***(mstari wa 50)*** kama ilivyo siku hizi, watu wanataka kuona ishara na miujiza ***(mstari wa 48)*** badala ya kupokea neno la Mungu kwa usalama wao: Imani kwanza kisha kuona!<br>3. **Matokeo.** Neno la Mungu li hai na kupitia neno tunaweza; si tu kumjua Bwana Yesu bali hata kutiwa nguvu nalo kwa kuwa nyuma ya neno la Mungu kuna nguvu ya Mungu. Yule diwani aliamini na kijana wake aliponywa na matokeo yake familia yake yote waliamini.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kuponywa kwa kijana |
| **REJELEA SOMO** | Jifunze Mstari Muhimu, ***Yohana 4: 50***, na jadili namna unavyoeleza kwa ufupi kwamba nguvu ya Bwana Yesu Kristo haikuleta uponyaji kwa mtoto wa diwani tu bali hata kwenye familia nzima ***(Yohana 4: 53)*** na ikamwamini Yesu. | Rejea kauli hii kutoka ***Waebrania 11: 6***; ‘Pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu’, na jadili namna inavyosadifu kile ambacho wanafunzi wamejifunza. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Sote tunahitaji kumwamini na kumtii Bwana Yesu kwa mioyo yetu yote ili tupate uzima wa milele.<br>2. Kama Wakristo wadogo tunapaswa kukubali kwamba Bwana Yesu hahitajiki kuwepo kimwili ili atende miujiza au kujibu maombi yetu kwa vile anaweza kufanya kusudi lake popote pale wakati wowote. Hii itutie moyo kwenye maisha yetu ya maombi. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Diwani alimwamini Bwana Yesu na alirudi nyumbani – alikuwa akitendea kazi imani yake. Fikiria njia ambazo imani yetu yaweza kuwekwa kwenye matendo nyumbani na shuleni.<br>2. Ni kwa namna gani kuweka imani yetu kwa Bwana Yesu kunaleta changamoto kwenye utamaduni ambamo tunaishi leo? (Rejea kwa watu ambao wanataka kuona kwanza na kisha waamini tofauti na kuamini kwanza kisha kuona mapenzi ya Bwana kwenye maisha yao kutoka katika neno lake). |

| | B2 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Tatu – Miujiza<br>Mada – Macho ya kipofu kufunguliwa | B2 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Tatu – Miujiza<br>Mada – Kipofu Bartimayo |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Marko 10: 46-52***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Marko 10: 52***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Bartimayo alikuwa na hitaji kubwa sana, alijua hitaji lake na alidhamiria Bwana Yesu akutane na hitaji lake.<br>2. Bwana Yesu aliyajibu maombi ya Bartimayo na Bartimayo alionesha shukrani zake kwa kumfuata Bwana Yesu katika safari yake ya mwisho kule Yerusalemu. | **Neno la Biblia:** ***Marko 10: 46-52***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Marko 10: 52***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Kama vile Bartimayo alivyoitwa ***(mstari wa 49)*** vivyo hivyo Bwana Yesu anawaita wale ambao ni vipofu wa kiroho kupitia Injili ihubiriwayo.<br>2. Tunapomwamini Bwana Yesu kwa ajili ya wokovu ni lazima tuyaache kabisa maisha yetu ya dhambi na tumfuate Yeye. |
| TOA UTANGULIZI | Waulize wanafunzi kama wanamfahamu mtu yeyote aliye kipofu na ongelea juu ya magumu anayokumbana nayo mtu wa jinsi hiyo. Jadili namna watu vipofu wanavyoweza wakasaidiwa, lakini upofu wa kimwili hauna tiba. | Elezea namna ilivyokuwa nadra sana kutoa msaada wowote kwa vipofu nyakati za Bwana Yesu na kwamba wengi walifanyika omba omba ili wapate kuishi. Tofautisha na hali ilivyo sasa. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Bartimayo kipofu, Myahudi aliaamini kuwa Yesu ni Masihi, mwana wa Daudi. Kwa ujumla Wayahudi hawakuamini swala hilo ***(11: 47)***<br>2. Bartimayo aliendelea kuita kwa sauti ili apate msaada wa kupata kuona tena, licha ya watu kumkemea anyamaze kimya. Bwana Yesu muumba mbingu na nchi na ndiye anayeshikilia ulimwengu, 'Alisimamishwa' ***(11: 49)*** na kilio cha omba omba akageuka akamtazama.<br>3. Bartimayo alionesha shukrani zake kwa kuwa mfuasi mwaminifu wa Yesu kwenye safari yake ya mwisho kuelekea Yerusalemu kabla ya kusulubiwa ***(11: 52)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Macho ya kipofu kufunguliwa. | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Bartimayo alikuwa kipofu na masikini pia, hii inatukumbusha kwamba tu vipofu kwenye mambo ya rohoni na kwa sababu hiyo hatujui mahali tunapo kwenda.<br>2. Hii ingeweza kuwa nafasi ya mwisho kwa Bartimayo kukutana na Bwana Yesu na kwa hiyo alimsihi sana Bwana "unirehemu" ***(mstari wa 47)***. Wokovu ni jambo binafsi kama linavyofafanuliwa na matumizi ya neno 'mimi'.<br>3. Bartimayo alitupilia mbali kila kitu ambacho kingemzuia kwenda kwa Bwana Yesu na kule kuomba kwake apate kuona alijibiwa haraka. Lilikuwa ni suala la 'upendo wa ghafla' kwa kuwa alimfuata Bwana Yesu mara. ***(mstari wa 50-52)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kipofu Bartimayo. |
| REJELEA SOMO | Wakumbushe maombi mafupi ya Bartimayo katika ***mstari wa 51*** na mwitikio wa haraka wa Yesu kwenye maombi hayo katika ***mstari wa 52***. Kama Yesu alivyomwuliza Bartimayo alitaka amfanyie nini, tunaweza kujifunza juu ya umuhimu wa kumtumainia Bwana Yesu na kisha kumfuata kwa kuwa nafasi ya kufanya hivyo inaweza kutopatikana wakati wote. Kama Bartimayo angeliikosa fursa hii pengine hangeliweza kukutana na Bwana Yesu tena. (Angalia kwenye ***Yohana 8: 12***) | Tazama ***Mathayo 4: 18-22*** na uwatafute wengine ambao waliacha mara moja kile walichokuwa wakifanya nao wakamfuata Bwana Yesu mara moja.<br>Tazama ***Waefeso 6: 10-18*** na ***Wakolosai 3: 8-17*** kutafuta ni viwango gani Bwana Yesu anategemea kwa wale wanaomfuata Yeye.<br>Kutokana na maandiko haya tengeneza orodha ya mambo sita muhimu ambayo yanaelezea maisha ya Mkristo. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Lazima Bwana Yesu alitiwa moyo kugundua kuwa Myahudi kipofu alikuwa na maono halisi ya kiroho na alikuwa amejiandaa kumfuata. Kila mtu anapaswa kumtumaini Bwana Yesu na kujaribu kumpendeza kwa kumfuata.<br>2. Maombi yetu si lazima yawe marefu. Tunaweza kumwambia Bwana Yesu kwamba tunampenda na kumwomba Yeye atuoneshe anataka tufanye nini kwa ajili yake.<br>3. Mwambie kila mtu aombe maombi mafupi kuhusu mahitaji yake binafsi. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Umuhimu wa kumtafuta Bwana Yesu kwa ajili ya wokovu wetu, bado anaendelea kutuita na bado muda upo.<br>2. Tunapokuwa wafuasi wa Bwana Yesu, nguvu zake zinafanya kazi ndani ya maisha yetu na tunaweza kutumiwa kwa kumpendeza Yeye na kwa kufanya mapenzi Yake.Tumeachana na maisha yetu ya dhambi na tumeanza maisha mapya na Bwana Yesu.<br>3. Soma ***Yohana 8: 12*** na fikiria nini maana ya kuacha giza la kale na 'kutembea katika nuru' |

<table>
<tr><th></th><th>B2 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Miujiza<br>Mada – Wakoma kumi kuponywa</th><th>B2 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Miujiza<br>Mada – Wakoma kumi</th></tr>
<tr><td></td><td>Neno la Biblia: Luka 17: 11-19<br><br>Mstari Muhimu: Zaburi 107: 8<br><br>Tunajifunza kuwa:<br>1. Bwana Yesu ndiye pekee anayeweza kututakasa dhambi zetu.<br>2. Wale wote waliotakaswa lazima waoneshe shukrani zao kwa kumtumikia Bwana Yesu kwa upendo na kwa kujitoa.</td><td>Neno la Biblia: Luka 17: 11-19<br><br>Mstari Muhimu: Waefeso 2: 8-9<br><br>Tunajifunza kuwa:<br>1. Sote tulizaliwa kama wenye dhambi na ugonjwa wa dhambi unaweza kuponywa na Bwana Yesu pekee.<br>2. Tunapokuwa tumeponywa ugonjwa wa dhambi kupitia imani katika Bwana Yesu, tunapaswa kumshukuru Yeye bila kukoma kwa ajili ya baraka ya wokovu na kwa mambo yote mema tunayoyapokea kutoka kwake kila siku</td></tr>
<tr><td>TOA UTANGULIZI</td><td>Elezea kwamba ukoma ni ugonjwa wa ngozi ambao huathiri idadi kubwa ya watu Duniani.<br><br>Rejea Mambo ya Walawi 13: 45-46 na elezea kwamba wakoma walikuwa wakichukuliwa kama watu ambao hawajatakasika kwenye kipindi cha Musa na walikuwa wakitengwa kwani walilazimika kukaa peke yao. Hili lilikuwa ni tatizo hata katika nyakati za Yesu.</td><td>Elezea kwamba ukoma ni ugonjwa unaoathiri sana ngozi ambao bado upo katika Ulimwengu wa leo. Inakadiriwa kuwa takribani watu milioni 20 wana huu ugonjwa. Baadhi yenu mnaweza mkawa mmesikia ‘The Leprosy Mission’ – shirika linalofanya kazi ya kuwasaidia watu ambao wana ugonjwa huu.<br><br>Taja watu wengine katika Biblia ambao waliugua ugonjwa huu wa ukoma. Angalia pia Mambo ya Walawi 13: 45-46.</td></tr>
<tr><td>KAMILISHA</td><td>Wasilisha Habari ya Biblia.<br><br>Jadili na uelezee:<br>1. Wakoma hawakuruhusiwa kuchangamana na watu. Kwa hiyo walipaza sauti zao wangali mbali kwa Bwana Yesu ili awarehemu. (17: 12-13)<br>2. Kwa kumtii Bwana Yesu, wakoma walishika njia kwenda nyumba za makuhani na walipofika huko walipona ukoma wao. (17: 14)<br>3. Makuhani ndio waliowapa ruhusa ya kurudi kwenye familia zao kulingana na sheria za wakati ule wa Agano la kale.<br>4. Ni mwenye ukoma mmoja tu, Msamaria, aliyerudi kumshukuru Yesu kwa kumponya.(17: 15-19)<br><br>Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.<br>Kamilisha Somo la Nne.<br>Onesha: Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Wakoma kumi kuponywa.</td><td>Wasilisha Habari ya Biblia.<br><br>Jadili na uelezee:<br>1. Wakoma hawakuweza kujiponya wenyewe lakini walikuja kwa mtu sahihi, Bwana Yesu kupata rehema (mstari wa 13)<br>2. Yesu aliposema ‘enendeni’ (mstari wa 14), wakoma walitii neno lake na walitakaswa wangali njiani kuelekea nyumbani kwa makuhani. Kutii na kuamini katika neno lililotamkwa na Bwana kulileta utakaso.<br>3. Mwenye ukoma mmoja, msamaria, kwa unyenyekevu alirudi kumshukuru na kumwabudu (mstari wa 16) Bwana Yesu kwa kupokea zawadi ya utakaso.<br><br>Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.<br>Kamilisha Funzo la Nne.<br>Onesha: Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Wakoma kumi.</td></tr>
<tr><td>REJELEA SOMO</td><td>● Rejea somo kwa kuonesha kwamba, ukoma ni picha ya mwenye dhambi aliye mbali kutoka kwa Yesu. Wakumbushe kila mmoja kwamba dhambi inaweza kutakaswa pale watakapomuita Bwana Yesu awasamehe dhambi zao na kuitii Injili. Injili huonesha kifo na kufufuka kwake Kristo<br>● Somo linatufundisha kwamba mara tunapotakaswa dhambi zetu ni lazima tuendelee kumshukuru Bwana Yesu kwa ajili ya wokovu wetu. Shukrani ni alama ya wale wanaompenda Bwana Yesu.</td><td>Wape wanafunzi maswali kwenye somo hili kama njia ya kulirudia na kujiandaa kujibu funzo la Wakati na Biblia.</td></tr>
<tr><td>LIISHI SOMO</td><td>Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:<br>1. Fikiria 1 Yohana 1: 9 na umuhimu wake.<br>2. Wakristo wanapaswa kumshukuru Bwana Yesu kwa kufa kwa ajili yao.<br>3. Kazi ya kikundi – tengeneza orodha ya vitu ambavyo tunapaswa kushukuru na andika maombi kulingana na mahitaji uliyonayo.</td><td>Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:<br>1. Fikiria kama wanafunzi wanafanana na wale wakoma tisa ama yule mmoja.<br>2. Jadili, kutoa shukrani kuna maana gani na ni jinsi gani kunaweza kuathiri maisha yetu. - Zaburi 40: 3<br>3. Kazi ya kikundi – tengeneza orodha ya vitu tunavyopaswa kushukuru na andika maombi kulingana na mahitaji uliyonayo.</td></tr>
</table>

| | B3 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Kwanza – Bethania<br>Mada – Dada wawili | B3 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Kwanza – Bethania<br>Mada – Nyumbani |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 10: 38-42***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 10: 42***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Bwana Yesu huthamini mahusiano yetu na Yeye zaidi ya huduma yetu.<br>2. Majukumu ya maisha yetu nyumbani ama shuleni, yasiruhusiwe kuingilia maisha yetu ya maombi na muda tunaotumia kusoma neno la Mungu. | **Neno la Biblia:** ***Luka 10: 38-42***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Marko 6: 31***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ili kukua na kuwa Wakristo imara, lazima tuchukue muda kutoka katika masumbufu yetu ya maisha na kusoma neno la Mungu tuweze kusikia ni nini Mungu anasema na sisi.<br>2. Ni lazima pia tutoe muda wetu kutoka katika masumbufu ya maisha yetu na kuomba ili kusudi tuweze kuongea na Mungu na kumshukuru Yeye kwa mema yake yote na tumuombe mwongozo wake kwenye maisha yetu. |
| TOA UTANGULIZI | Waambie wanafunzi wafikirie jinsi inavyoleta heshima mtu muhimu kama vile kiongozi mkubwa kutembelea nyumbani kwao.<br>Nyumba ya Mariamu na Martha ilikuwa ni moja ya nyumba pekee ambayo Yesu aliitembelea.<br>Kila mmoja ahamasishwe kufikiri baadhi ya nyumba zingine ambazo Yesu alitembelea:<br>***Luka 4: 38, Luka 7: 37, Luka 8: 51, Luka 19: 5.***<br>Nyumba zetu zinapaswa kuwa mahala ambapo Bwana anaheshimiwa na kutiiwa. | Elezea kwamba Mariamu na Martha wote walimpenda Yesu. Katika tukio hili wote walikuwa wakihusika na kumhudumia. Martha hakutambua kwamba kwa kujishughulisha sana alikuwa hakika anampuuza mgeni wake yaani Bwana Yesu. Hakuwa na muda wa kumsikiliza na kujifunza kutoka kwake.<br>Waambie wanafunzi ni vipaumbele vipi vipo kwenye maisha yao.<br>Wapime na hakikisha wanaelewa 'kujishughulisha' sio mbadala wa maombi ama kusoma Biblia. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Wakati Martha alipokuwa "akitenda kazi" Mariamu alikuwa "akiabudu'. Kazi pamoja na kuabudu ni lazima viende sambamba. *Jadili nini maana ya kuabudu.*<br>2. Ingawa Martha alitamani kumheshimu Yesu kwa mambo mbalimbali, Yesu alisema, "jambo moja linahitajika" ina maana jambo moja lilikuwa latosha. Alikuwa anapendelea sana kuwa na ushirika pamoja nao kwa kuwa alisema Mariamu 'amechagua fungu jema' ***(mstari wa 42)***. Chakula kwa ajlili ya maisha yetu ya kiroho ni cha muhimu sana kuliko kile cha mwili na Bwana Yesu alitaka Mariamu na Martha kwa pamoja watambue jinsi ilivyo muhimu kusikiliza Neno Lake ***(1 Petro 2: 2)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Dada wawili. | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Bwana Yesu alilenga shabaha yake kwenye maombi na kusoma Biblia kama mambo makubwa mawili ya msingi yenye baraka katika maisha yetu.<br>2. Yesu hakumlaumu Martha kwa kujishughlisha na mambo ya kazi za ndani bali kwa upole alimsahihisha kwa kutokuwa na vipaumbele sahihi.<br>3. Bwana Yesu anaonesha katika ***mstari wa 42*** kwamba kumsikiliza Yeye ni jambo muhimu zaidi kwake. Anapendezwa na upendo wetu kwake zaidi ya huduma zetu. Bwana anataka sisi tutoke kwenye kuwa 'akina-Martha' na kuwa 'akina-Mariamu'.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Nyumbani. |
| REJELEA SOMO | Inafurahisha kuona kuwa Mariamu "alikaa miguuni pa Yesu". ***(mstari wa 39)*** Jadili kwamba kwa kuchukua nafasi hii ya chini na unyenyekevu Mariamu alikuwa akimpa Bwana Yesu hadhi na heshima aliyoistahili.<br>1. Waambie juu ya njia ambazo nasi pia tunaweza kumpa hadhi na kumheshimu Bwana Yesu katika maisha yetu.<br>2 Watu katika maandiko yafuatayo walionekana kukaa miguuni pa Yesu.Kwa mfano - ***Mathayo 28: 9, Marko 5: 22, Luka 7: 38, Luka 8: 35.*** Tazama mistari hii na utawaona ni akina nani hawa na jadili umuhimu wao kuwa miguuni pa Yesu. | Tumia andiko muhimu kusaidia kurudia somo hili kwa kuonesha kuwa:<br>1. Kuna muda mwafaka kumsikiliza Bwana Yesu. ***(Marko 6: 31)***<br>2. Kuna muda sahihi wa kumfanyia kazi Bwana Yesu. ***(Marko 6: 7-13) (Warumi 12: 1)***<br>3. Bwana Yesu ameahidi kuwabariki wale wote ambao huduma zao zinaambatana na maisha yao ya maombi bila kukoma. ***(Yohana 15: 5)*** |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1 Kuwa na uwiano mzuri kati ya kazi zetu binafsi na muda wa kuabudu katika maisha yetu ya kila siku?<br>2. Kuishi katika namna ambayo inamletea Yeye heshima na furaha?<br>3. Kujali zaidi kuhusu 'kutumika vyema' kuliko 'kutumika sana'?<br>4. Kuhakikisha kwamba kazi haitangulii usomaji wa Biblia zetu na muda wa maombi?<br>5. Fikiria juu ya nafasi na kipaumbele anachohitaji Yesu kuwa nacho kwenye maisha yetu. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kuhakikisha tunakuwa na uwiano sawa kwenye muda wetu kwa kutenga muda wa maombi na kusoma Biblia kuwa vipaumbele vya kila siku.<br>2. Kuhakikisha hatupotezi maana ya utumishi wetu kwa Bwana Yesu kiasi cha kumtumikia kama tunaofanya shughuli zetu za kawaida ambazo hazina maana kwake. |

| | **B3 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Pili – Bethania**<br>**Mada – Huzuni kuwa furaha!** | **B3 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Pili – Bethania**<br>**Mada – Akiwa Kaburini** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Yohana 11: 1-7 na 17-44***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 11: 25***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Bwana Yesu pekee ndiye anaweza kumfufua aliyekufa akawa hai tena.<br>2. Bwana Yesu pekee ndiye anayeweza kuwapa uzima wa milele watu wenye dhambi ambao wanaelezewa na mtume Paulo kama “wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zao” ***(Waefeso 2: 1)*** | **Neno la Biblia:** ***Yohana 11: 1-44***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 11: 25-26***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Kufufuliwa kwa Lazaro na Bwana Yesu kutoka katika wafu ulikuwa ni udhihirisho mzuri wa nguvu za Yesu juu ya kifo na ufufuo ni msingi wa imani ya Kikristo. Sio tu kwamba Yesu alikuwa na nguvu ya kujifufua Yeye mwenyewe ***(Yohana 10: 18)*** bali pia kuwafufua wengine.<br>2. Yesu alilia hadharani ***(mstari wa 35)*** kuonesha kwamba anajali kiasi cha kulia pamoja nasi katika majaribu na huzuni zetu. |
| **TOA UTANGULIZI** | Waambie wanafunzi wakumbuke baadhi ya miujiza aliyofanya Yesu na jadili ni miujiza ipi inayodhaniwa ni mikubwa zaidi.<br>Huu ulikuwa ni muujiza wa mwisho wa huduma ya Bwana Yesu kufanyika hadharani. Baadhi ya Wayahudi walihoji kwa nini Bwana Yesu aliruhusu Lazaro afe wakati alikuwa na uwezo wa kumponya kipofu ***(mstari wa 37)*** Angeweza kufanya hivyo lakini kwa kumfufua Lazaro kutoka kwa wafu, alikuwa akionesha ukweli na uwezo wa maneno yake katika ***mstari wa 25***: “ Mimi ndimi huo ufufuo na uzima” | Anza somo hili kwa kuelezea kwamba kufufuka kwa Lazaro kutoka kwa wafu, ni muujiza wa mwisho kati ya miujiza saba katika Injili ya Yohana, uliwashawishi Wayahudi wengi waliokuwepo juu ya ukweli kwamba, Yesu alikuwa ni mwana wa Mungu na walimwamini ***(11: 45)***. Ingawa baadhi ya Wayahudi ambao pia wakuwepo na kushuhudia muujiza huu hawakuamini na walipeleka taarifa kwa Mafarisayo juu ya kilichotokea Bethania. Walikuwa pengine waliotafuta njama za kumuua Bwana Yesu. ***(11: 46)***. Washauri wanafunzi kuwa ndivyo ilivyo hata sasa. Kuna wale ambao wanakubali kwamba Bwana Yesu alikuwa Mungu na wapo pia wanaokataa hili na wanakataa ukweli kwamba alitenda miujiza. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Nyumba ya Martha, Mariamu na Lazaro kule Bethania ilikuwa ni moja ya nyumba ambazo Bwana Yesu alipendelea kuwapo. Wanafunzi waweze kuulizwa ikiwa kama Bwana Yesu yupo kwenye nyumba zao, mioyo ama kwenye maisha yao. ***Ufunuo 3: 20***.<br>2. Kama vile Bwana Yesu alivyomfufua Lazaro kutoka katika wafu, anaweza pia kuwapa maisha mapya ya kiroho yanayodumu milele wale ambao wamekufa kiroho.<br>3. Habari hii inatuonesha kuwa Bwana Yesu ni Mwokozi mwenye huruma, ‘Yesu alilia’ ***(mstari wa 35)*** na Wayahudi katika kipindi hicho waliweza kuona namna gani Yesu alivyompenda Lazaro. ***(mstari wa 36)*** Aliwapenda pia wao lakini wengi wao hawakulifahamu hili.<br>4. Wakati Yesu alipomwita Lazaro atoke kaburini, alipata maisha mapya; alifunguliwa kutoka mavazi ya kaburini ya kufungwa sanda ***(mstari wa 44)*** na alikuwa ushuhuda unaoishi wa nguvu za Bwana Yesu katika maisha yake.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Huzuni kuwa furaha! | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mariamu na Martha walimwomba Yesu awasaidie kumfufua kaka yao aliyekuwa amekufa kwa sababu walikuwa wameona miujiza yake. ***(11: 1-3)***<br>2. Yesu aliipenda familia hii lakini hakuitikia mwaliko wao haraka. Lazaro alikufa ili kusudi nguvu ya Yesu juu ya mauti ipate kuonekana kwa wanafunzi wake na Wayahudi wengine waliokuwapo. ***(11: 5-6)***<br>3. Yesu alilia kwa sababu aliguswa na tukio la kumpoteza Lazaro ***(11: 35)***<br>4. Yesu alimwita mtu aliyekwishakufa naye alisikia na kuitika! ***(11: 43-44)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Akiwa Kaburini. |
| **REJELEA SOMO** | 1. Kama vile Lazaro alivyopewa maisha mapya ***(mistari ya 44-45)*** vivyo hivyo wale wote wanaomwamini Bwana Yesu wanapewa maisha mapya. Tazama kwenye ***Wakolosai 2:13*** na ***2 Timotheo 1: 10***, kuona jinsi ambavyo Bwana Yesu anaweza kuwapa ‘maisha mapya’ wenye dhambi ‘waliokufa’.<br>2. Kama vile maisha mapya ya Lazaro yalivyokuwa uthibitisho wa nguvu ya Bwana Yesu katika utendaji kwenye maisha yake, ndivyo Bwana Yesu, anavyowapa wale wote wanaomwamini Yeye nguvu ya kuishi katika Yeye. ***(Waefeso 2: 10)*** | Rudia somo kwa kuainisha majaribu mbalimbali kwenye maisha yetu na jinsi Bwana Yesu anavyoweza kuleta mazuri kutoka kwenye hali mbaya. Rejea ***Warumi 8: 28***. Kukawia kwa Bwana kunaweza kutufanya tufikirie kwamba Bwana hajali na hajibu maombi yetu lakini ni lazima tujifunze kuwa wavumilivu na kila mara kumwamini Yeye kwa sababu hawezi kutuacha ama kutuangusha. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Juu ya toba binafsi na kurudi kwa Bwana Yesu ‘kutembea katika upya wa uzima’? ***(Warumi 6: 4)***<br>2. Juu ya kuwa watii wa neno la Mungu kwa kuwashirikisha wengine Injili, kuwa mwanafunzi mhamasishaji, kuwa mtii kwa wazazi na pengine kwa kubatizwa? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Wakristo wana maisha ya kiroho ambayo mauti haiwezi kuyashinda wala kuyafuta. Uhakika huu utufanye sisi kutaka kuishi maisha ya kujitoa kwa Bwana Yesu. ***Wafilipi 1: 21-23***.<br>2. Katika muujiza huu Bwana Yesu anatuonesha kuwa anatujali kiasi cha kulia na sisi katika huzuni zetu. |

| | B3 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Tatu – Bethania<br>Mada – Safari nyingine | B3 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Tatu – Bethania<br>Mada – Akiwa chakulani |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Yohana 12: 1-11***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Yohana 4: 19***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Pale tunapompenda Bwana Yesu kweli, tunapata namna ya kuonesha shukrani zetu kwake.<br>2. Kamwe tusijaribu kuchelewa kufanya tunachoweza kumfanyia Bwana Yesu kwa kuwa hatujui tutakuwa na muda mrefu au mfupi kiasi gani wa kumtumikia. | **Neno la Biblia:** ***Yohana 11: 55-57; 12 :1-11***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Zaburi 95: 6***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Hakuna kitu cha thamani mno cha kumpa Bwana Yesu. Anastahil vyote vizuri tulivyo navyo!<br>2. Ikiwa kama tunampenda Bwana Yesu, tutatembea katika utii wa maelekezo ambayo ametupa kama yalivyoainishwa kwenye Agano Jipya. |
| TOA UTANGULIZI | Elezea jinsi Bethania palivyokuwa mahali pa kumbukumbu maalumu kwa Bwana Yesu.<br>Wakumbushe wanafunzi kuwa katika nyumba ya Martha na Mariamu, ndipo Bwana Yesu alipofundisha umuhimu wa kuabudu.<br>Katika somo la 2 Yesu alionesha kuwa alikuwa ni 'Ufufuo' pale alipomfufua Lazaro.<br>Katika somo hili Bwana Yesu yupo mezani katika nyumba hii ya Bethania. | Tukio hili katika ***Yohana 12: 1-11*** ni mjumuisho wa wazo lile lile kama lilivyo katika ***Marko 14: 3-9***. Bwana Yesu alimsifu Mariamu kwa kile kitendo cha kumsujudia kwa kumpaka ile marhamu ya thamani miguuni pake bila uchoyo.<br>Marhamu na marashi vilitumika sana kwenye kuzika miili ya wafu – soma ***Mwanzo 50: 2-3***.<br>Yesu anajibu kitendo cha Mariamu cha kujitolea katika ***mstari wa 7*** kwa kuonyesha kuwa yalikuwa ni maandalizi ya maziko Yake. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Ni heshima waliyokuwa wamepewa Martha, Mariamu na Lazaro ya kuwa pamoja na Bwana Yesu, wakila chakula na kufurahia urafiki wao pamoja na Yesu ***(mstari wa 2)***<br>2. Fursa aliyokuwa amepewa Mariamu ya kuipaka miguu ya Bwana Yesu kwa marhamu ya thamani na kuifuta kwa nywele zake ***(mstari wa 3)***, ni kutuonesha kwamba hakuna kitu cha thamani sana cha kumpa Yeye na kwamba anastahili maisha yetu zaidi.<br>3. Pale Yuda alipolalamika kwamba marhamu hiyo ingeliuzwa na pesa wakapewa maskini ***(mstari wa 5)***, Bwana Yesu alimkumbusha kwamba maskini wangeendelea kuwepo duniani kwa ajili ya wengine kuwaonesha wema. Hata hivyo, fursa ya kutumia mafuta haya kwa Bwana Yesu ingekuwa adimu kwa kuwa Yesu alikuwa akielekea msalabani kufa kwa ajili ya wenye dhambi.<br>4. Wakuu wa makuhani walitaka kumuua Lazaro. ***(mstari wa 10)*** Nadhani inaweza kuwa ni kwa sababu wao waliukataa ufufuo na walitaka kumuua Lazaro kwa kuwa yeye alikuwa ni ushahidi kwamba Bwana Yesu ni ufufuo na uzima.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Ttu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Safari nyingine. | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. **Nyumba**- Rejea ukweli kwamba nyumba ya Bethania ***(mstari wa 1)*** ilikuwa ni mahali pa (i) Huduma na maelekezo; (ii) kuabudu na ushirika; na (iii) kufa na kufufuka.<br>2. **Sikukuu** ***(mstari wa 2)*** ilikuwa 'kwa ajili Yake.' Mariamu, Martha na Lazaro walikuwa na kila sababu ya kukutana naye kama mgeni rasmi.<br>3. **Kupaka mafuta** ***(mstari wa 3)*** ilionesha Mariamu alimpenda Bwana Yesu kwa kuwa upendo unapimwa kwa sadaka.<br>4. **Pongezi** ***(mstari wa 7-8)*** ilikuwa ya juu mno kutolewa na Yesu na alionesha kitendo hiki cha kuabudu kingeendelea kuwa kumbukumbu/historia – soma ***Mathayo 26: 13***.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Akiwa chakulani. |
| REJELEA SOMO | Habari hii inaelezwa pia katika ***Marko 14: 3-9***. Soma ***mstari wa 8*** kubaini ni nini Bwana Yesu alimwambia huyu mwanamke aliyempaka miguu yake mafuta.<br>Soma maneno ya Mathayo kuhusu habari hii katika ***Mathayo 26: 6-13***, uone kuwa Bwana Yesu hakutabiri tu kuhubiriwa kwa Injili baada ya kifo chake bali pia kwamba kitendo alichotenda mwanamke huyu kitatajwa kwa kumbukumbu lake. | Waulize wanafunzi maswali pale unaporejea Funzo hili, maswali ambayo yatawasaidia kutoa majibu sahihi kwenye maswali yaliyoulizwa kwenye Funzo la 3. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je upendo wako kwa Yesu una nguvu kiasi gani kuwahamasisha wengine?<br>2. Wayahudi wengi walimwamini Bwana Yesu ***(mstari wa 11)*** kwa sababu waliweza kuona ushahidi wa nguvu zake katika maisha mapya ya Lazaro. Je ni kwa namna gani unaweza kuwahamasisha wengine wamwamini Bwana Yesu kupitia maisha yako, ikiwa unampenda Yeye? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. **Nyumba** – Je Bwana Yesu yupo nyumbani kwetu kwa namna yoyote kama inavyotajwa hapo juu kwenye namba 1?<br>2. **Sikukuu** – Kwa Wakristo, je Bwana Yesu ni mtu wa kwanza kwenye maisha yetu?<br>3. **Kupaka mafuta** – Ni kwa kiwango gani tunampenda Bwana Yesu? Je tunampa vilivyo vya thamani kwetu?<br>4. **Pongezi** – Bwana Yesu alisema kuwa Mariamu alifanya aliyoweza. ***(Marko 14: 8)*** |

| | B3 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Bethania<br>Mada – Katika mji wa Yerusalemu | B3 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Bethania<br>Mada – Njiani kwenda Yerusalemu |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 19: 28-44***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 1: 12***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Wakati Yesu anaingia Yerusalemu, wafuasi wake wanaimba kwa sauti, wanamsifu kwa kazi zake kubwa alizowafanyia miongoni mwao.<br>2. Yesu anaulilia mji wa Yerusalemu kwa sababu watu walimkataa na hawakumpa nafasi. | **Neno la Biblia:** ***Luka 19: 28-44***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 1: 12***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ni jambo muhimu sana kumkaribisha Bwana Yesu sasa, ndani ya mioyo na maisha yetu kwa kuwa ipo siku hatutaweza kupata fursa hii adhimu.<br>2. Bwana Yesu anapendezwa tukitumia imani, upendo, kuabudu, huduma na mali zetu kwa sifa na utukufu wake ikiwa kama sisi tu mali yake. |
| TOA UTANGULIZI | Toa wazo kuwa 'Jumapili ya Mitende kabla ya Pasaka' haikutokea kwa bahati mbaya. Ilikuwa imetabiriwa miaka mingi kabla.<br>Rejea kitabu cha ***Zakaria 9: 9*** ambapo kelele za kuja/ kuingia kwake Bwana Yesu zilitabiriwa takribani miaka 500 kabla ya tukio lenyewe kutokea. | Anza Funzo hili kwa kuonesha kwamba Bwana Yesu aliulilia mji wa Yerusalemu ***(mistari ya 41-42)*** kwa kuwa walikuwa wamekosa nafasi yao ya kumpokea kama Masihi wao jambo ambalo lingemaanisha kuleta amani kwao. Sasa walikuwa wamechelewa na Bwana Yesu anawaonya juu ya hatari inayolikabili taifa la Wayahudi miaka ya mbele.<br>Kama Bwana Yesu alivyotabiri katika mwaka 30 BK, ***(Luka 19:43-44)*** Jenerali wa Kirumi, Tito, aliuteka mji wa Yerusalemu (70 BK) na kuliharibu Hekalu na kuwaua wakazi wake. Bwana Yesu alitembelea mji wa Yerusalemu ili kuwapelekea wokovu lakini hawakumpa nafasi na ndipo uharibifu ulipowajia. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Kuingia kwa shangwe ***(mstari wa 28-40)*** kwa Bwana Yesu mwanzoni mwa wiki la kusulubiwa kwake.<br>2. Wanafunzi walipiga kelele za sifa. ***(mstari wa 37)*** Kumbuka walipaza sauti wakisema "amani juu mbinguni" na si "amani duniani" kwa sababu kifo cha Bwana Yesu na kupaa kwake kungeleta "amani mbinguni". Kusingekuwa na "amani duniani" kwa kuwa walikuwa wanataka kumuua Bwana Yesu – Mfalme wa Amani.<br>3. Yesu anaulilia mji wa Yerusalemu kwa sababu ya watu wake kumkataa Yeye na sasa wamechelewa – walikuwa wameikosa nafasi yao. ***(mstari wa 42)***<br>4. Yesu anaonesha kuwa katika mwaka 70 BK, chini ya Tito, Jenerali wa Rumi, Yerusalemu na watu wake wataharibiwa kwa sababu hawakujua 'majira ya kujiliwa kwao'. ***(mstari wa 44)***, ikimaanisha kuwa Bwana Yesu aliwaletea wokovu lakini wakaukataa.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Katika mji wa Yerusalemu. | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. **Kuingia Yerusalemu** - Bwana Yesu aliingia Yerusalemu juu ya mwana-punda aliyeazimwa, kama ilivyotabiriwa katika ***Zekaria 9: 9***. Wale walioshuhudia maandamano ya ushindi wa Yesu katika Yerusalemu walimwona Yesu kama utimizo wa unabii huu uliotabiriwa zaidi ya miaka 500 kabla ya kutokea. ***(Luka 19:35-36)***<br>2. **Wakati wa Kuingia Yerusalemu** - Yesu alichagua wakati ambapo Israeli wote wangekusanyika Yerusalemu kwa ajili ya Sikukuu ya Pasaka.<br>3. **Matumaini ya Watu -** Watu walikuwa wakimsifu Mungu kwa kuwapa mfalme ambaye walimtarajia kuwa kiongozi wa kitaifa. Hata hivyo, walipotambua kuwa alikuwa akisimamisha ufalme wa milele wakawa kinyume naye. ***(Luka 19:38)***<br>4. **Mwitikio wa Mafarisayo -** Mafarisayo walipinga Yesu kuheshimiwa hadharani na kumtaka awanyamazishe watu wake na Yesu anawakemea kwa kuwa wagumu kuliko mawe! ***(Luka 19:39-40)***<br><br>**Eleza Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A - Njiani kwenda Yerusalemu. |
| REJELEA SOMO | Rejea habari na jadili umuhimu wa kumwamini Bwana Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wetu sasa. Rejea ***2 Wakorintho 6: 2***, kwa kuwa kesho twaweza kuwa tumechelewa. Pia fikiria namna ile hukumu itakavyoujilia ulimwengu kama ilivyokuwa kipindi cha Tito katika mwaka 70 BK, ambapo wale watakaokuwa hawana muda na Bwana Yesu watakuwa wamepotea. | Rejea Funzo hili kwa kuliweka katika mazingira ya maisha ya Yesu. Yerusalemu kulikuwa ni kitovu cha nguvu ya dini, dola na makazi ya Wayahudi na magavana wa Kirumi. Matukio mengi muhimu ya maisha ya Yesu yalitukia hapo ikiwa ni pamoja na kusulubiwa na kufufuka. Wiki yake yote ya mwisho aliitumia hapo. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Fikiria ina maana gani kuacha dhambi na kumwamini Bwana Yesu kwa ajili ya wokovu.<br>2. Mstari Muhimu unaelezea wale wote ambao wamempokea Bwana Yesu kama: 'wana wa Mungu.' Fikiria vifungu vingine ambavyo vina watu wengine ambao wamempokea Bwana Yesu wanaofahamika. (mfano, Mkristo nk.) | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Uzima wa milele bado unapatikana kwa wale wanao-ukubali, wakati nafasi bado ingalipo<br>2. Fikiria njia ambazo Bwana Yesu anaweza kuzihitaji katika maisha yetu kama katika ***Luka 19: 31***.<br>3. Kama vile unabii katika ***Zekaria 9: 9*** ulivyotimia, vivyo hivyo unabii kuhusu Ujio wa Pili wa Bwana Yesu utatimia. |

| | B4 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Kwanza – Bwana Yesu<br>Mada – ‘Kufa kwake’ | B4 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Kwanza – Bwana Yesu<br>Mada – Kufa kwake |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 23: 1-26 na mistari ya 32-46***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 23: 33***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alikufa ili dhambi zetu ziweze kusamehewa.<br>2. Ili kufika mbinguni ni lazima tugeuke kwa kutubu dhambi zetu na kumwamini Bwana Yesu. | **Neno la Biblia:** ***Luka 23: 32-56***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 15: 13,14***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ili kuingia mbinguni tunahitaji kukubali kuwa, sisi tu wenye dhambi, tunastahili adhabu ya Mungu.<br>2. Tena tunahitaji kuamini kuwa Bwana Yesu alikuwa hana dhambi na alibeba adhabu kwa niaba yetu. |
| **TOA UTANGULIZI** | Anza somo hili kwa kuwauliza wanafunzi wanaelewa nini kuhusu umuhimu wa Pasaka. Elezea kwamba somo hili linaeleza habari ya Pasaka ya kwanza.<br>Jadili jinsi somo hili linavyotuonesha kuwa watu wote hawaendi mbinguni. Wanyang’anyi wawili walisulubiwa pia pamoja na Bwana Yesu, mmoja alikwenda mbinguni na mwingine hakwenda. | Kwa kiifupi fafanua matukio yaliyomfikisha hadi msalabani, kiwa ni pamoja na kukamatwa, majaribu na safari ya kuelekea Kalvari.<br>Jadili namna somo hili linavyoonesha kuwa wokovu umejengwa juu ya toba na imani na namna ambavyo yule mhalifu aliyetubu aliingia mbinguni na yule mhalifu ambaye hakutubu hakuingia. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Pilato hakuona hatia yoyote ndani ya Yesu lakini alimhukumu kufa ili kuwapendeza watu. ***(mistari 1-7, 13-25)***<br>2. Ingawa Pilato na Herode walikuwa ni maadui, wakawa marafiki na wote walikuwa upande mmoja kinyume na Bwana Yesu ***(mstari wa 12)***<br>3. Masaa sita ya kusulubiwa (saa tatu asubuhi hadi saa tisa alasiri) Yesu msalabani akiwa katikati na wanyang’anyi pembeni mwake ni utimilifu wa ***Isaya 53: 12***.<br>4. Kulikuwa na wanyang’anyi wawili ***(mstari wa 39-43)*** lakini ni mmoja pekee alikwenda mbinguni. Sisitiza kwenye ***mstari wa 43***: ‘leo’ – kasi gani! -‘pamoja nami’ – uhusiano gani! ‘ paradiso’ – furaha iliyoje!<br>5. Masaa matatu ya giza ***(mstari wa 44-46)*** na pazia la hekalu kupasuka vipande viwili kuonesha kwamba Yesu ni njia ya kwenda kwa Mungu. ***(Waebrania 10: 19-20)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza. Mstari huu unaelezea somo kwa ufupi lakini 1 Petro 3: 18a unaweza kuwa mstari mzuri zaidi kukumbuka**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kufa kwake. | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Masaa sita ya kusulubiwa katika kutimiza ***Isaya 53: 12*** - (saa tatu asubuhi mpaka saa tisa alasiri).<br>2. Habari ya mnyangányi aliyetubu ***(23:42- 43)*** inaonesha kuwa wokovu umejengwa juu ya toba na imani. Mtu huyu aliingia mbinguni lakini alikuwa kamwe hajabatizwa wala kushiriki sakramenti.<br>3. Wanyang’anyi wawili ni wawakilishi wa watu – wale ambao wanampenda Bwana Yesu na wale walio maadui zake.<br>4. Kipindi cha masaa matatu ya giza ***(mstari was 44-46)*** Yesu alibeba adhabu ya dhambi zetu na kupitia mauti yake na njia ya kumkaribia Mungu ilikuwa imefunguliwa kwa wote wamjiao kwa imani.<br>5. Habari hii inaonesha ***(mstari wa 50-56)*** kwamba ingawa Yusufu alikuwa mwanafunzi wa siri, alikuwa ni rafiki wa kweli wa Bwana Yesu, kama walivyokuwa wanawake waaminifu waliotajwa, kwa namna ambavyo tunaona akimfanyia Bwana Yesu mazishi ya heshima.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br><br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kufa kwake. |
| **REJELEA SOMO** | Rejea somo kwa kuwaambia wanafunzi wasome ***Isaya 53: 12*** ujumbe ambao uliandikwa zaidi ya miaka mia moja kabla ya kifo cha Bwana Yesu na kisha rejea Biblia ilivyoandikwa kwa pumzi ya Mungu.<br>Wakiwa katika vikundi waandike baadhi ya vichwa vya magazeti kuelezea tukio la msalabani. | Rudia somo kwa kuwaambia wanafunzi wasome kitabu cha ***Isaya 53*** ambacho kiliandikwa zaidi ya miaka 700 kabla ya kifo cha Bwana Yesu na jadili namna kinavyowasilisha kitabu cha ***Luke 23: 32-56***. Kazia kwamba Biblia ni kitabu chenye pumzi ya Mungu.<br>Wakiwa katika vikundi watengeneze orodha ya baadhi ya nabii zilizotajwa katika kitabu cha ***Isaya 53*** ambazo zilitimizwa msalabani. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Namna gani twaweza kuwa na uhakika kuwa dhambi zetu zimesamehewa?<br>2. Sote tunakumbana na changamoto. Je, sisi tupo upande upi? Upande wa wale wanaompenda Bwana Yesu au upande wa wale ambao ni maadui zake?<br>3. Je unawezaje kumjibu mtu ambaye anasema kila mtu atakwenda mbinguni? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Sote twakabiliwa na changamoto ya ama kuwa rafiki au adui wa Yesu.<br>2. Kama tunampenda Bwana Yesu kama Yusufu tutatafuta namna ya kuonesha upendo wetu. Twawezaje kuuonesha?<br>3. Unawezaje kumjibu mtu ambaye anasema sote tunakwenda mbinguni? |

| | B4 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Pili – Bwana Yesu<br>Mada – Kufufuka kwake | B4 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Pili – Bwana Yesu<br>Mada – Kufufuka kwake |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Yohana 20: 1-18***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Warumi 10: 9***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Baada ya siku tatu ndani ya kaburi, Bwana Yesu akafufuka.<br>2. Mariamu Magdalena alionesha upendo wake kwa Bwana Yesu. | **Neno la Biblia:** ***Luka 8: 1-3, Yohana 20: 1-18***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Warumi 10: 9***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Bwana Yesu alishinda kifo pale alipofufuka tena.<br>2. Mariamu Magdalena alikuwa mfuasi wa Bwana Yesu mwenye bidii.<br>3. Fikiria ufufuo kama ukweli ambao una ushahidi mwingi kwenye Biblia. |
| **TOA UTANGULIZI** | Jadili maana ya 'ufufuo' na waambie wanafunzi kubaini mtu yeyote ambaye Bwana Yesu alimfufua kutoka kwa wafu (Lazaro – ***Yohana 11: 44***, Binti Yairo – ***Luka 8: 55***). Fikiria kwamba nguvu ya ufufuo ni ya Bwana Yesu. | Jadili namna nguvu ya ufufuo inavyotoka kwa Bwana Yesu na bainisha mtu yeyote ambaye alimfufua kutoka wafu. (Lazaro – ***Yohana 11: 44***, Binti Yairo ***Luka 8: 55***). Pia ainisha namna wale ambao wamekwisha kufa baada ya kumwamini Bwana Yesu watafufuliwa hapo baadaye. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mariamu Magdalena, Petro na Yohana waliona, walishuhudia ufufuo – kaburi wazi. ***(Yohana 20 :1-8)***<br>2. Petro na Yohana walirudi nyumbani lakini Mariamu Magdalena aliendelea kusimama peke yake yake nje ya kaburi akilitazama. ***(Yohana 20: 10-18)***<br>3. Bwana Yesu alimtuza Mariamu Magdalena kwa kujitoa kwake kwa kumtokea Yeye binafsi na elezea kwamba mara atakaporudi tena mbinguni, atamtuma Roho wake Mtakatifu kukaa ndani ya mioyo ya waamini.<br>4. Anamtuma kwenda kuwapasha habari wanafunzi wake kwamba Yu Hai na kwamba lazima wakutane naye Galilaya. ***(Mathayo 28: 10)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kufufuka kwake. | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mariamu Magdalena alimtumikia Bwana Yesu enzi za uhai wake na alithibitisha bidii yake kwa kuwa wa kwanza kufika katika kaburi lililokuwa wazi ***(Luke 8: 1-3)***<br>2. Mariamu Magdalena, Petro na Yohana waliona ushahidi wa kufufuka kwake na pia waliona mpangilio mzuri wa mavazi ya kaburini kuonesha kuondoka kwa Bwana Yesu kulipangiliwa na hakukurupuka na hivyo kukanusha madai kuwa mwili ulikuwa umeibwa. ***(Yohana 20: 3-9)***<br>3. Bwana Yesu aliimtuza Mariamu Magdalena kujitoa kwake kwa kumtokea yeye mwenyewe na kumwambia kuwa atakaporudi tena mbinguni, atamtuma Roho Mtakatifu akae ndani ya mioyo ya waamini. ***(Yohana 20: 10-18)***<br>4. Anamwambia aende na kuwaambia wanafunzi kwamba Yu hai na lazima wakutane naye Galilaya. ***(Mathayo 28: 10)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kufufuka Kwake. |
| **REJELEA SOMO** | Unganisha somo hili na maandiko yafuatayo katika Agano Jipya pale ambapo Bwana Yesu alitangulia kusema habari za ufufuo wake. Jadili umuhimu na manufaa ya ufufuo.<br>● ***Mathayo 16: 21, 17: 22-23, 20 :18-19***<br>● ***Luka 18: 31-33, 24: 7***<br>● ***1 Wakorintho 15: 3-4*** | Unganisha somo hili na ***1 Wakorintho 15: 3-8, 12-20*** na onesha namna ***mstari wa 4*** una rejea ***Isaya 53: 9*** na ***Zaburi 16: 9-10***.<br>Jadili watu tofauti waliomwona Bwana baada ya kufufuka kwake. ***(1 Wakorintho 15: 5-8)*** na kwa nini ufufuo ni muhimu sana. ***(1 Wakorintho 15: 17)*** |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Umuhimu wa wanafunzi kusema wanampenda Bwana Yesu kama Mwokozi wa maisha yao.<br>2. Tafakari namna upendo wetu kwake, unavyopaswa kubadilisha maisha yetu.<br>3. Ni muhimu pia kujifunza kutoka katika somo hili umuhimu na uhakika wa ufufuo. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Fikiria umuhimu wa maisha binafsi na upendo kwa Bwana Yesu.<br>2. Ufufuo ni muhimu kwenye imani ya Mkristo kwa kuwa kama ingelikuwa Kristo hakufufuka, kifo chake kingelikuwa ni bure na tusingeliweza kuwa na tumaini la kuwa mbinguni milele. |

| | B4 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Tatu – Bwana Yesu<br>Mada – 'Kuondoka kwake' | B4 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Tatu – Bwana Yesu<br>Mada – Kupaa kwake |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Yohana 20: 19-31; Luka 24: 45-53***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 24: 51***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu anaposema nasi jambo fulani kupitia Biblia, huwa tunamfurahisha kwa kulitii.<br>2. Kusudi la Injli ya Yohana ni kwamba wale wanaoisoma wapate kuamini na kuwa na uzima wa milele. | **Neno la Biblia:** ***Luka 24: 45-53; Matendo 1: 1-12***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 24: 51***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Bwana Yesu anataka wale walio wake wawe mashahidi wake katika ulimwengu huu.<br>2. Siku moja Yesu atakuja tena duniani kuwachukua walio wake kwenda nao Mbinguni. |
| **TOA UTANGULIZI** | Jadili kwa mifano halisi, namna gani tunavyoamini vitu vingi ambavyo hatujaviona au kuvishika. Elezea namna ambavyo imani ya Mkristo haijajengwa kwenye kuona bali kwa kuliamini neno la Mungu na Bwana Yesu. | Jadili jinsi tunavyopenda kuyatii maneno ya mwisho yanayosemwa na wale tuwapendao hususani kabla hawajafa. Fikiria baadhi ya maneno ya mwisho ya watu mashuhuri katika historia wanapokufa. Husianisha hili na maneno ya mwisho ya Bwana Yesu. ***(Matendo 1: 8-9)*** |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Jadili kuhusu Yesu alivyowatokea wanafunzi wake na unukuu maneno yake kwao 'Amani iwe kwenu'. ***(mstari wa 21)*** Elezea kwamba kutokana na 'kifo cha Bwana Yesu' wale wote waliomwamini kwa imani wana amani ya kweli. ***(Warumi 5: 1)***<br>2. Yesu alishughulika na Tomaso mwenye imani haba kwa upole na alimshawishi kuwa Yeye ndiye Yesu aliyefufuka. (***Yohana 20: 27-28)***<br>3. Tomaso alijibu kwa maneno ya imani na uwajibikaji.<br>4. Kutoka katika mlima wa mzeituni Bwana Yesu aliondoka kwenda mbinguni siku arobaini baada ya kufufuka kwake, baada ya hapo wanafunzi wake walirudi hekaluni kumsifu na kumshukuru Mungu kwa ufufuo wake na kungojea kurudi kwake tena. ***(Luka 24: 50-53)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kuondoka kwake. | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Bwana Yesu aliwaamuru wanafunzi wake wawe mashahidi ***(Matendo 1: 8)*** wake Yerusalemu, katika nchi ya Palestina na Ulimwenguni kote.<br>2. Bwana Yesu alipaa mbinguni kutoka Mlima Mizeituni ***(Matendo 1: 12)*** na atarudi tena kwenye Mlima Mizeituni. ***(Zekaria 14: 4)***<br>3. Alipaa akiwa anaonekana kimwili. Siku moja atakuja tena katika mwili ***(Malaki 3: 1)*** na mwenye kuonekana. ***(Mathayo 24: 30)***<br>4. Aliinuliwa juu mawinguni kwa nguvu na utukufu na atarudi tena juu ya mawingu mbinguni kwa nguvu na utukufu. ***(Mathayo 24: 30)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kupaa Kwake. |
| **REJELEA SOMO** | Jifunze Mstari Muhimu na jadili namna unavyolielezea somo kwa ufupi. Wakumbushe wanafunzi kwamba wanafunzi wa Yesu pia walikuwa wakitazamia utimilifu wa ahadi waliyoahidiwa kuhusu ujio wa Roho Mtakatifu. ***(Luka 24: 49)*** | Angalia rejea za Biblia katika pointi 1-4 hapo juu halafu linganisha na tofautisha kurudi kwake Bwana Mbinguni baada ya ufufuo Wake na Kurudi Kwake mara ya pili duniani. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Ni namna gani tunaweza kumwamini Bwana Yesu kwa ajili ya wokovu ingawa hatujawahi kumwona?<br>2. Bwana Yesu aliwatia moyo wanafunzi wake kufanya kazi yake mara baada ya Yeye kupaa. Ni kazi ipi twaweza kumfanyia?<br>3. Tazama ***Matendo 1: 8.*** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Namna gani waamini katika Bwana Yesu wanaweza kumshuhudia nyumbani, shuleni au miongoni mwa marafiki?<br>2. Fikiri juu ya watu ambao wameacha makwao kuwa wamisionari maeneo mengine duniani.<br>3. Wanafunzi waweze kushirikisha shuhuda zao binafsi kwamba ni kwa namna gani wamemwamini Bwana Yesu kama Mwokozi na Bwana. |

| | B4 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Bwana Yesu<br>Mada – ‘Kurudi kwake’ | B4 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Bwana Yesu<br>Mada – Kurudi kwake |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 1: 4; 8-12***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 1: 11***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Nguvu ya Roho Mtakatifu inahitajika tunaposhuhudia ama kuhubiri Injili.<br>2. Bwana Yesu ambaye alipaa mbinguni, atarudi tena duniani kuwachukua wale walio tayari kuwa pamoja naye mbinguni. | **Neno la Biblia:** ***Yohana 14: 1-6; Matendo 1: 9-11***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Wathesalonike 4: 16-17***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Kurudi kwa Bwana mara ya pili ni tukio ambalo ni hakika litatokea ingawa siku wala saa haijulikani.<br>2. Katika kurudi kwake mara ya pili, waliokufa katika Kristo watafufuliwa na kupelekwa Mbinguni pamoja na Wakristo walio hai wakati huo. |
| TOA UTANGULIZI | Ongelea juu ya shahidi labda wa ajali ambaye ameona ama kusikia kabisa kilichotokea. Wanafunzi waseme kutokana na uzoefu wao kuhusu Bwana Yesu.<br>Fikiria pia kwamba nguvu waliyoipata wanafunzi ili kuwafanya wao kuwa mashahidi wa Bwana Yesu ni nguvu hiyo hiyo tumeipokea pia pale tulipoacha dhambi na kuamini kile ambacho Bwana Yesu alikifanya kwa ajili yetu pale msalabani kuchukua dhambi zetu. Sisi nasi tunaweza na tunapaswa kuwa mashahidi. | Wakumbushe wanafunzi kuwa nabii zote kutoka Agano la Kale kuhusu kuja kwa Bwana duniani kama mwanadamu zilishatimia, vivyo hivyo nabii zote kuhusu kuja kwake kwa mara ya pili zitatimia.<br>Jadili na wanafunzi namna ambayo mtu tunayempenda anapokwenda mbali tunavyongojea kwa shauku kurudi kwake na namna ambayo wale wanaomwamini Bwana Yesu wanavyotakiwa kungojea kurudi kwake. Angalia ***Tito 2: 13***. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Bwana Yesu aliwaagiza wanafunzi wake kuwa mashahidi wake kwanza Yerusalemu kisha katika nchi ya Palestina na mwisho wa dunia yote. ***(Matendo 1: 8)***<br>2. ‘Watu wawili wenye mavazi ya kung’aa’ ambao wanawake waliokuja kaburini waliwaona, ***(Luka 24: 4)*** waliwaambia kaburi lilikuwa wazi na Bwana Yesu alikuwa amefufuka. Inawezekana walikuwa ni malaika wale wale katika namna ya kibinadamu ambao sasa walikuwa wakiwaambia wanafunzi kuhusu kuja kwake mara ya pili. ***(Matendo 1: 10-11)***<br>3. Kurudi kwake kutafanana na kupaa kwake.<br>4. Siku ya kurudi kwake haijulikani, kwa hiyo ni muhimu sana kujiweka tayari. ***(Matendo 1: 7)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kurudi kwake. | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Watu wawili ‘wenye nguo nyeupe’ ***(Matendo 1: 10-11)*** waliwaambia wanafunzi juu ya kuja kwa Bwana duniani kwa mara ya pili. Elezea kuwa inawezakana kabisa watu hawa wawili ndiyo walewale malaika katika ***Luka 24: 4*** ambao walimwambia yule mwanamke aliyekuwa kaburini kuhusu ufufuo.<br>2. Linganisha ahadi ya Bwana katika ***Yohana 14: 3*** na ***Matendo 1: 11*** na elezea Maandiko yalivyo kweli na yenye pumzi ya Mungu.<br>3. Soma ***1 Wathesalonike 4: 16-17*** na elezea mafunuo ya ajabu aliyokuwa nayo Paulo juu ya kuja mara ya pili. Elezea kama ifuatavyo:<br>Kuna sauti ya kusikia – kelele na tarumbeta;<br>Macho ya kuona – Bwana pekee;<br>Muujiza wa kuhisi – unyakuo;<br>Mkutano wa kuufurahia – ‘kumlaki Bwana mawinguni’;<br>Na faraja tutakayoipata – ‘kuwa na Bwana’ milele.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kurudi kwake. |
| REJELEA SOMO | Fungua mistari ifuatayo na onesha jinsi Bwana alivyosema juu ya ujio wake kama ‘mwivi ajavyo usiku’ kwa sababu hakuna ajuae ni lini mwivi atakuja. Matokeo yake ni uhitaji wa kumwamini Yeye kwa ajli ya wokovu wetu na kuwa tayari na kusubiri ujio wake. ***Mathayo 24: 44, Luka 12: 20.*** | Ujio wa mara ya pili hauna mashaka kwa wale ambao wameokolewa na wako tayari kumlaki Bwana. Biblia inatufundisha kwamba Wakristo watazamie kurudi kwake na waishi katika namna inayompendeza. Rejea ***Tito 2: 11-14***, na ***1 Yohana 3: 2-3***. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kila mtu anahitaji kufikiria kama yuko tayari kwenda mbinguni kama Bwana atakuwa anakuja sasa.<br>2. Ni nini lingekuwa jibu la mtu ambaye anasema muda bado upo mwingi wa kujiandaa kwenda mbinguni, kutokana na kile ulichojifunza juu ya ujio wake mara ya pili?<br>3. Ni lini muda mwafaka wa kuwa tayari kwenda mbinguni? Rejea ***2 Wakorintho 6: 2.*** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Wakristo wanapaswa kuishi maisha ya haki kutokana na kukaribia kurudi mara ya pili kwa Bwana Yesu ili awakute wakiwa waaminifu wakati wa kuja kwake. Je hii inamaanisha nini?<br>2. Wale wasioamini wataachwa wakati wa kuja kwake mara ya pili. Je namna gani habari hii ya kusikitisha inatupa changamoto kama Wakristo kwa ajili ya kuwashuhudia wengine? |

| | **B5 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Kwanza – Watumwa wa Bwana**<br>**Mada – Kuandaliwa na Mungu** | **B5 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Kwanza – Wakristo wa kwanza**<br>**Mada – Stefano** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 1: 7-9; Matendo 2: 1-13***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 14: 16-17***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Katika siku za mwanzo za kanisa la Wakristo, Bwana Yesu aliwaamuru mitume waende kuhubiri Injili katika maeneo yao na ulimwenguni kote.<br>2. Kama Roho Mtakatifu alivyoshuka na kukaa ndani ya mioyo ya mitume ndivyo wale wote wanaomwamini Bwana Yesu watakavyokuwa na uwepo wa Roho Mtakatifu na nguvu ya kuwasaida katika maisha yao ya Ukristo. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 6: 1-15; 7: 54-60***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 6: 8***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ni watu wenye tabia ya Stefano wanaobadilisha ulimwengu kwa ajili ya Mungu<br>2. Ni Wakristo wa kweli tu kama Stefano ambao wana maanisha kutangaza kweli ya Injili na wanajali sana kile kinachompendeza Mungu kuliko yale ambayo watu wanaweza kusema au kuwafanyia. |
| **TOA UTANGULIZI** | Waambie wanafunzi wafikiri jinsi wanafunzi wa Yesu walivyojisikia baada ya Yesu kupaa mbinguni, na wakati Roho Mtakatifu aliposhuka siku ya Pentekoste.<br>Elezea namna gani Matendo ya Mitume inabeba maudhui makuu mawili:<br>1. Bwana Yesu, ambaye sasa amepaa, anatenda kazi kupitia wale waliopo katika dunia hii yaani waliomwamini kwa Roho wake Mtakatifu.<br>2. Ufufuo na kuinuliwa kwa Bwana Yesu mawinguni bado ni kiini cha ujumbe wakati kitabu hiki kilipokuwa kikiandikwa miaka ya 60-67 BK. | Jadili mateso yana maana gani na fikiria kuhusu mifano ya zama hizi za kisasa..<br>Elezea kuwa nyakati za Wakristo wa kwanza viongozi wa dini walikuwa na ushawishi mkubwa sana kwenye serikali/dola na Wakristo walikuwa wamejiandaa kwa upinzani wao lakini mara zote kwa staha na heshima. Wakristo waliheshimu na kutii serikali ya kipindi hicho isipokuwa tu pale sheria za wanadamu zilipokinzana na sheria za Mungu. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mstari muhimu katika kitabu hiki ni ***Matendo 1: 8*** na Matendo yote yameelezewa kulingana na maeneo ambapo Injili imeenea:<br>Mashahidi ndani ya Yerusalemu – ***Sura ya 1-7***<br>Mashahidi Yudea – ***Sura ya 8: 1-4***<br>Mashahidi Samaria – ***Sura ya 8: 5-25***<br>Mashahidi Ulimwenguni kote – ***Sura ya 8: 26***<br>2. Siku ya Pentekoste ***(2: 1)*** ilikuwa ni siku pekee ambayo Roho Mtakatifu alishuka ili kukaa na Waamini siku zote - Alikuja kukaa. Walijazwa Roho Mtakatifu ***(2: 4)***. Tunapomwamini Bwana Yesu Roho Mtakatifu anakaa ndani mwetu lakini ili kujazwa Roho Mtakatifu, ni lazima tusome Biblia zetu, tutumie muda katika kuomba na kuishi maisha ya kumtii Bwana.<br>3. Bwana Yesu aliweka msingi imara kwenye kazi iliyokamilika ya msalaba na sasa anawawezesha waamini, kupitia Roho wake Mtakatifu kuwa mashahidi na wasaidizi katika kuieneza habari njema ya kifo, ufufuo na ujumbe wa wokovu kwa wote. Roho Mtakatifu anatajwa kama 'mfariji au mshauri' katika Mstari Muhimu wa ***Yohana 14: 16*** unaoonesha kuwa Bwana Yesu pia ni mwombezi au msaidizi wetu.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kuandaliwa na Mungu. | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Stefano alikuwa na viwango ambavyo vinapaswa kuonekana kwenye maisha ya Wakristo - ukweli, kujazwa Roho Mtakatifu, kujawa imani na nguvu, hekima na shauku ya kumtumikia Bwana Yesu. ***(Angalia Matendo 6: 3,5 & 8)***<br>2. Upinzani kwenye huduma ya Stefano yenye nguvu uliibuka kutoka jamii ya Wayahudi waliokuwa ndani ya Masinagogi au jirani na Yerusalemu. Ingawa wakati Stefano alipotokea mbele ya Baraza, baraza la Wayahudi, walimshtaki mashtaka ya uongo; na waliuona utukufu wa Bwana Yesu uking'aa usoni mwa Stefano. ***(Matendo 6: 15)*** Stefano alijitetea kwa ustadi ***(Matendo 7: 1-53)*** na aliwakosoa vikali viongozi wa Kiyahudi, akiwashutumu kwa kumpinga Roho Mtakatifu na kisha kuhusika na kumsulubisha Bwana Yesu.<br>3. Lazima Stefano alikuwa amejua maisha yake yalikuwa hatarini lakini akawa tayari kufa kuliko kumsaliti Bwana wake. Mara tu baada ya kushuhudia kuwa anaona 'mbingu zimefunguka' ***(Matendo 7: 56)*** umati ulimtoa nje ya mji na kumpiga kwa mawe hadi kufa. ***(Matendo 7: 57-58)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Stefano. |
| **REJELEA SOMO** | Dk Luka, mwandishi wa kitabu cha Matendo ya Mitume anaanza kwa kuonesha 'yale yote ambayo Yesu alianza kuyatenda na kuyafundisha' katika ***Matendo 1: 1***. Katika ***Matendo 28: 31*** Paulo bado anahubiri habari njema. Fikiria kuwa kitabu cha Matendo ya Mitume bado kinaendelea - kazi ya Uinjilisti haijakamilika mpaka Bwana atakaporudi kuwachukua wale wanaomwamini. | Jadili namna maandiko haya yanavyotoa muhtasari wa somo hili:<br>1. ***2 Timotheo 2: 3*** – 'Ushiriki taabu kama askari mwema wa Kristo';<br>2. ***1 Petro 4: 14*** - "Mkilaumiwa kwa ajili ya jina la Kristo ni heri yenu;kwa kuwa Roho wa utukufu na wa Mungu anawakalia." |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kwa sisi waamini, Roho Mtakatifu anakaa ndani mwetu. Ni jukumu letu 'kujazwa Roho Mtakatifu' Soma ***Waefeso 5: 18***<br>2. Kujifunza masomo ya Wakati na Biblia kunapaswa kukuhimiza: - Kusoma Biblia na kuomba. Tendea kazi yale unayosoma na mwongozo unaopewa na Bwana katika maisha yako ya kila siku. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kama vile Stefano alivyouawa kwa ajili ya imani yake katika kufa na kufufuka kwa Bwana Yesu, Wakristo wengi wanakuwa wakiteswa, hata kuuawa, katika baadhi ya nchi leo hii kwa imani hiyo hiyo.<br>2. Tunapaswa kumwomba Bwana Yesu katika maombi yetu kutufanya watiifu na waminifu kwake pasipo kujali ni mazingira gani yanaweza kutokea katika maisha yetu. |

| | B5 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Pili – Watumwa wa Bwana<br>Mada – Kuandaliwa kufa! | B5 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Pili – Kanisa la Kwanza<br>Mada – Filipo |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 6: 1-5, 8-15; 7: 54-60***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 5: 44***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Stefano alikuwa mwaminifu kwa mambo madogo kabla ya kutumiwa na Mungu, kama inavyoelezwa kwenye huduma ya mezani ***(Matendo 6: 2)***, kabla ya kufanya ishara na miujiza mikubwa. ***(Matendo 6: 8)***<br>2. Stefano ni kama Bwana Yesu kwa kuwa alikuwa ni mwaminifu na mtu asiye na lawama, mtu aliyekuwa tayari kuyatoa maisha yake kwa ajili ya Injili. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 6: 5; 8: 4-17; 8: 26-40.***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 8: 35***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Filipo alikuwa mhubiri wa Injili aliyefanikiwa na ambaye alikuwa tayari kuacha uamsho Samaria na kwenda jangwani hadi Gaza kuhubiri Injili kwa mtu mmoja mhitaji.<br>2. Mara alipomwamini Bwana Yesu kuwa Mwokozi wake, Mwethiopia alikuwa ana shauku ya kumtii Bwana katika ubatizo na alikuwa na furaha kuu moyoni mwake alipokuwa akirudi nyumbani. |
| TOA UTANGULIZI | Fikiria kuhusu mateso unayopata kutokana na imani yako yanamaanisha nini na toa mifano ya nyakati za sasa.<br>Eleza namna ambavyo Wakristo wa kwanza walisonga mbele na Injili, wakikumbana na upinzani kutoka kwenye serikali zao na viongozi wa dini wa enzi hizo. Ingawa waliwaheshimu na kuwatii watawala wao, walikuwa tayari kutokutii sheria za wanadamu pale zilipokuwa zinakinzana na sheria ya Mungu hata kufikia hatua ya kuyapoteza maisha yao. | Filipo alikuwa ni mmoja wa watu saba waliochaguliwa katika ***Matendo 6: 5*** kuangalia maswala ya kanisa. Baadaye alikuwa mwinjilisti na alipeleka Injili Samaria. Alipokuwa angali katikati ya uamsho huko Samaria, Bwana alimwita aende Gaza, nchi ya jangwani kukutana na mgeni mhitaji kutoka Kushi (Ethiopia), kwa nia ya kumtumia Filipo kwa ajili ya wokovu wa mtu huyo na ubatizo. Mara baada ya hili kukamilika Filipo aliondolewa kwa namna ya ajabu na kuendelea na kuhubiri Injili maeneo mengine. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Tabia ya Stefano inaelezewa kama Mkristo ambaye amejawa Roho Mtakatifu, na maisha mazuri na ya ukweli. ***(Matendo 6: 3)*** yaliyojaa imani, nguvu ***(Matendo 6: 8)*** na hekima ***(Matendo 6: 10)*** na ambaye alikuwa na bidii kwenye kazi ya Bwana. ***(Matendo 6: 8)***<br>2. Alipokamatwa bila kosa na viongozi wa Kiyahudi, Stefano alijitetea kwa kuwakumbusha washitaki wake kwamba taifa la Wayahudi sio tu waliendelea kumkataa Bwana Yesu bali pia kosa lao kubwa lilikuwa ni kumsulubisha 'mwenye haki' . ***(Matendo 7: 52)***<br>3. Ingawa alizungukwa na umati wa wenye hasira waliompiga kwa mawe hata kufa, Stefano kama Bwana Yesu alikabidhi roho yake kwa Bwana. ***(Matendo 7: 59)*** na akaomba kwa ajili ya waliomuua kisha 'akalala'. ***(Matendo 7: 60)*** Neno 'akalala' mahala hapa linamaanisha mwili wake 'umelala mpaka Bwana atakaporudi kwa ajili ya Kanisa Lake.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kuandaliwa kufa! | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Filipo alikuwa mtii wa agizo la Mungu kwenda na kuhubiri Injili kwa Mkushi.<br>2. Mkushi alikuwa ametoka Afrika kuja Yerusalemu kuabudu lakini aliondoka pasipo uelewa sahihi wa Injili. Alirudi kwenye maandiko kutafuta msaada. ***(8: 27-28)***<br>3. Filipo kwa kuelekezwa na Bwana, alifika kwa muda mwafaka na kumfafanulia Isaya 53. Alimwonesha jinsi hiyo sura ilivyokuwa ikihusu maisha na kifo cha Bwana Yesu. ***(8: 34-35)***<br>4. Mkushi alimwamini Bwana Yesu na alibatizwa mara moja kwa kuzamishwa majini na akarudi nyumbani akiwa na furaha ***(8: 36-38)***<br><br>**Elezea mstari muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Filipo. |
| REJELEA SOMO | Hakikisha wanafunzi wanajifunza Mstari Muhimu. Jadili pamoja nao namna gani unaelezea kwa kifupi somo hili na jinsi gani linahusiana na wote wawili; Yesu na Stefano; eleza kwamba wote waliomba kwa ajili ya waliowaua ***(Luka 23: 34 na Matendo 7: 60)*** na wote walikabidhi roho zao kwa Mungu ***(Luka 23: 46 na Matendo 7: 59)*** | Unganisha funzo hili na ***Isaya 53***. Onesha jinsi ambavyo sura hii ilikuwa imeandikwa kati ya miaka 740-680 KK na jinsi ambavyo unabii wa Isaya ulitangulia kuelezea kwa usahihi kabisa kuhusu kufa, kuzikwa, kufufuka na kuinuliwa kwa Bwana Yesu Kristo. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Katika kipindi kigumu, inawezekana kuwa mwaminifu kwa Bwana Yesu?<br>2. Namna gani kujitolea kwa Stefano kwa Bwana kunatoa changamoto kwenye kujitolea kwetu leo, wakati baadhi ya sheria zilizotungwa na Serikali zinapingana kabisa na Maandiko Matakatifu? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Pale Yesu anapotuita kufanya kazi yake, tunatii pasipo kuuliza kama Filipo alivyofanya?<br>2. Je tunaliishi namna gani jukumu letu kama Wakristo katika kujaribu kuwa mashahidi wazuri wa Bwana Yesu katika kuwaona wengine wakija kwa Yesu?<br>3. Wanafunzi wametambua kuwa ubatizo ni njia ya kuonesha imani yao hadharani? |

| | B5 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Tatu – Watumwa wa Bwana<br>Mada – Kuandaliwa kusikiliza! | B5 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Tatu – Kanisa la kwanza<br>Mada – Kornelio |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 8: 1-5; 26-40***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 16: 31***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mwitikio na utii usio na mashaka wa Filipo ulisababisha Bwana amtumie kumleta Mkushi (Mwethiopia) kwa Bwana.<br>2. Mkushi (Mwethiopia) alikwenda zake akifurahi kutokana na utii wake kwa Bwana. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 10: 1-8; 23-48***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 10: 43***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Injili ni kwa ajili ya wote, Wayahudi na Mataifa.<br>2. Kornelio na nyumba yake walikuwa ni miongoni mwa Wamataifa wa kwanza kumwamini Bwana Yesu. |
| TOA UTANGULIZI | Elezea kwamba, wakati mwingine Mungu anatutaka kufanya kitu fulani ambacho ni tofauti kabisa na vile tunavyotarajia kufanya.<br>Eleza kwamba Filipo alikuwa anaona kazi kubwa ikifanywa kwa ajili ya Bwana huko Samaria. Hata hivyo, alielekezwa na Bwana kuondoka mahali ambapo wengi walikuwa wakiongoka na kwenda eneo la jangwa la Gaza ili kuwa msaada wa kiroho kwa mtu mmoja tu, yaani mtu kutoka Ethiopia. | Elezea kwa kifupi mazingira yalivyokuwa kati ya Wayahudi na Wamataifa, na namna ilivyo kawaida kwa Wayahudi kuwa na mahusiano madogo na hivyo kutokwenda kabisa kwenye nyumba za Wamataifa.<br>Kornelio alikuwa afisa wa Kirumi (Mmataifa), akida ambaye aliishi katika mji wa Kaisaria na alikuwa mtu maarufu katika kazi yake ya uaskari. Ingawa alikuwa akiishi maisha ya unyofu hakumjua Bwana Yesu japokuwa alikuwa akitafuta kwa bidii msamaha wa dhambi zake na Mungu aliliona hili na kiasi kwamba alikutana na Petro ambaye alimhubiria Injili yeye na familia yake. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Wakati Filipo anakutana na Mwethiopia, anasoma ***Isaya 53: 7-8*** na Filipo anapata nafasi ya kuzungumza naye juu ya maisha na kifo cha Bwana Yesu.<br>2. Mwethiopia alijifunza kutoka kwa Filipo kwamba mtu ambaye Isaya aliandika habari zake alikuwa ni Bwana Yesu aliyekufa msalabani kuwa Mwokozi wake na Mwethiopia alitambua kuwa ni mwenye dhambi na akampokea Bwana Yesu Kristo kama Mwokozi wake kwa kumwamini. ***(Matendo 8: 34-38)***<br>3. Filipo alielezea umuhimu wa kubatizwa kwa Mwethiopia na walipofika karibu na mahali penye maji, Filipo akambatiza. Watumishi waliosafiri na Mwethiopia hawakushuhudia tu ubatizo wake bali waliona pia jinsi gani Mwethiopia alivyojaa furaha sasa kwa sababu alikuwa ni mfuasi wa aliyejulikana kuwa Yesu Mnazareti katika kipindi kile.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kuandaliwa kusikiliza! | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Siku moja Kornelio aliona maono wazi wazi majira ya saa 9 alasiri ambapo malaika wa Mungu alimtokea na kumwambia atume watu Yafa wamwite Petro ***(10: 3-6)***<br>2. Petro alipokuja nyumbani mwa Kornelio kulikuwa na watu wengine pia waliokuja kumsikiliza akihubiri. ***(10: 24)***<br>3. Petro alilieleza kundi kwa kuwaambia kwanza Mungu hakuwa na upendeleo – Wokovu ulikuwa ni kwa wote Wayahudi na Mataifa. ***(Matendo 10: 34-35)***<br>4. Petro alihubiri kwa wale waliokuwepo juu ya maisha, kifo na kufufuka kwa Bwana Yesu Kristo na alimaliza kwa kuwaambia waupokee msamaha wa dhambi. ***(10: 38-44)***<br>5. Hivi ndivyo Mataifa waliokuwepo walifanya na walikuwa ni miongoni mwa Mataifa wa kwanza kumwamini Bwana Yesu na kubatizwa. ***(Matendo 10: 47-48)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kornelio |
| REJELEA SOMO | Unganisha somo hili na ***Isaya 53*** na jadili hususani ***mistari ya 7 na 8***. Kama mwana kondoo anyamazavyo mbele ya wao wakatao manyoya yake, Bwana Yesu aliustahimili msalaba. Hakupewa jaribu rahisi na alikufa angali kijana mdogo na alikufa kwa dhambi zetu. | Fikiria nafasi ya Petro kama Myahudi kuingia nyumba ya Mmataifa. Tazama ***Matendo 10: 9-17*** kuona jinsi Petro alivyopewa maelekezo ya namna gani afanye, na namna gani anapaswa kufikiria juu ya kupeleka Injili kwa Mataifa. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kuelewa kwamba Mkristo mtiifu anaweza kuleta baraka halisi kwenye maisha ya wengine – wote walio Wakristo na wasio Wakristo.<br>2. Imani binafsi kwa Bwana Yesu lazima ifuatiwe na kubatizwa. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kufahamu kwamba msamaha wa dhambi unapatikana kwa wote, bila kujali rangi, utamaduni au dini.<br>2. Jadili ukweli kwamba kwa sasa tuna Biblia ya kutuelekeza nini cha kufanya katika maisha yetu na namna dhambi zetu zinavyoweza kusamehewa? |

| | B5 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Mtumwa wa Yesu<br>Mada – Kuandaliwa kwenda! | B5 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Kanisa la Kwanza<br>Mada – Barnaba |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 10: 1-20; 24-29; 33-43***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 10: 43***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Licha ya Kornelio kuwa mwema, alihitaji mtu wa kumwambia namna ambayo angeweza kuwa Mkristo.<br>2. Petro alijifunza, kutokana na maono yake kuwa Injili haikuwa tu kwa ajili ya Wayahudi bali ni kwa ajili ya kila mmoja. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 4: 32-37; 9: 26-31; 11: 19-30***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 11: 24***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Hatuwezi kufanyika Wakristo kwa kufanya yaliyo mema.<br>2. Wakristo wanafanya yaliyo mazuri kwa sababu 'wema' ni moja ya tunda la Roho Mtakatifu ndani ya maisha ya Mkristo. ***(Wagalatia 5: 22)*** |
| TOA UTANGULIZI | Somo hili linatoka Kaisaria, mji ulioko pwani. Kornelio alikuwa afisa wa jeshi la Rumi na kama akida alikuwa juu ya kikosi cha watu mia moja. Alikuwa pia anahusiana na kikundi cha jeshi la Italia. Hata hivyo, alikuwa ni mtu aliyekuwa akimtafuta Mungu. Alikuwa ni Mmataifa lakini mpaka hatua hii Petro alikuwa amepeleka Injili kwa Wayahudi wenzake tu. | Tunatambulishwa Barnaba kwa mara ya kwanza katika ***Matendo 4: 36***. Maana ya jina lake ni 'mwana wa faraja'. Anatoka katika kisiwa cha Kipro na Biblia inatuambia kuwa aliuza shamba lake na alileta pesa na kuwapa mitume. Alikuwa akiliishi jina lake kwa kuwa, ukarimu wake ulikuwa ni faraja kwa mitume. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Malaika alimwambia Kornelio katika maono atume watu kwenda Yafa mji ulio kusini mwa Kaisaria wamwite Simoni Petro.***(Matendo 10: 3-6)***<br>2. Siku iliyofuata, Petro aliona maono akiwa juu ya dari ya nyumba ya Simoni alipokuwa amekwenda kusali. Mungu alimfunulia Petro kuwa Injli haikuwa ni kwa ajili ya Wayahudi tu bali ilikuwa kwa ajili ya Wamataifa pia. Mungu huona matabaka mawili tu ya watu – wale walio wake na wale wasio wake! ***(Matendo 10: 9-16)***<br>3. Petro alipoingia nyumbani kwa Kornelio, alikiri kwamba aliamini upendeleo wa Mungu ulikuwa ni kwa ajili ya taifa la Israeli, Wayahudi lakini akajifunza: Mungu hana upendeleo. ***(Matendo 10: 34-35)***<br>4. Petro alihubiri Injili kwa wale waliokuwepo na alisisitiza wokovu ulikuwa ni kwa 'kila mmoja aliye mwamini Yesu'. ***(Matendo 10: 43)***<br>5. Wale waliokuwepo waliamini na kubatizwa na huu ukawa mwanzo wa Mataifa kuingia katika kanisa.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza..**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kuandaliwa kwenda! | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Barnaba alikuwa mtumwa wa Yesu mwenye bidii kwa kuwa hakuwa mbinafsi. Alitumia muda wake na mali ili kwamba na wengine wasaidike. Alitaka kuona watu wanakuja kumjua Bwana Yesu na alitaka kuwasaidia wale wote waliokuwa kwenye uhitaji wa mahitaji ya msingi ya maisha. Matokeo yake alijulikana kama 'mtu mwema'. ***(Matendo 11: 24)***<br>2. Barnaba alionesha wema kwa Paulo. ***(Matendo 9: 27)*** Alimtetea Paulo pale Wakristo wa Yerusalemu walipoogopa kumpokea.<br>3. Barnaba alitumwa na kanisa la Yerusalemu kuwatia moyo kanisa jipya la Antiokia na alipokuwa kule wengi walimgeukia Bwana. Aliwatia moyo Wakristo wapya wa Antiokia 'kuwa wa kweli kwa Bwana'' ***(Matendo 11: 23)*** Pengine hapakuwepo na maneno ya hekima yaliyosemwa kwa waamini wapya!<br>4. Barnaba alipokuja Antiokia na kuona yote yaliyokuwa yanatokea, alitambua kuwa alihitaji msaidizi kwa hiyo alikwenda Tarso na kumpata Sauli ambaye angemsaidia. ***(Matendo 11: 25-26)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Barnaba. |
| REJELEA SOMO | Jifunze Mstari Muhimu na jadili namna unavyoeleza kwa kifupi somo letu la leo. Pia warejeze wanafunzi kwenye kishazi kinachosema, 'amwaminiye' - ***Yohana 3: 15-16***. | Rudia funzo kwa kuuliza maswali ambayo yatawawezesha wanafunzi kujibu maswali katika Funzo la 4 kwa usahihi. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kushirikisha Injili kwa vijana wa mataifa mengine?<br>2. Elezea ***Matendo 10: 34-35*** kwa maneno yako mwenyewe. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kuonesha 'wema' katika maisha yetu kama Wakristo?<br>2. Kuwa wakweli kwa Bwana Yesu kama Wakristo?<br>3. Kuwatia moyo Wakristo wengine ambao wanapita katika wakati mgumu. |

| | B6 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Kwanza – Maisha ya Yusufu<br>Mada – Kijana mwota ndoto | B6 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Kwanza – Yakobo na familia yake<br>Mada – Wakiwa Harani |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 37: 1-11***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 37: 8***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Wakati Yusufu angali kijana mdogo wa miaka 17, Mungu alisema naye katika ndoto na akamfunulia kuwa alikuwa na mpango na maisha yake.<br>2. Dhambi ya wivu haimpendezi Mungu na inaweza kuendelea kuwa dhambi ya hatari zaidi na hivyo lazima iepukwe. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 29: 1-30***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Wagalatia 6: 7***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yakobo amemdanganya baba yake na kaka yake na kulazimika kukimbilia kwa mjomba wake huko Harani ili kuokoa maisha yake<br>2. Mungu anatawala kila kitu na muda wake ni mkamilifu.<br>3. Tukipanda matendo ya dhambi maishani mwetu, tutegemee kuvuna matokeo yake |
| **TOA UTANGULIZI** | Wakumbushe wanafunzi juu ya watangulizi wa Yusufu; Ibrahimu, Isaka na sasa tunakuja kwa Yakobo na familia yake. Yusufu alikuwa ni mmoja wa watoto wa Yakobo na jina la mama yake lilikuwa ni Raheli. Kazi ya Yusufu ilikuwa ni kuchunga kondoo. Alikuwa na mdogo wake aliyeitwa Benyamini na ilikuwa katika kumzaa Benyamini ambapo Raheli alikufa.Yakobo alikuwa na wake wanne lakini Raheli alikuwa ni kipenzi chake na ndiyo maana watoto wake wawili Yusufu na Benyamini walikuwa pia ni wapendwa kwa Yakobo. | Wakumbushe wanafunzi juu ya watangulizi wake Yakobo. Yakobo alikuwa mtoto wa Isaka na Rebeka na Esau alikuwa kaka yake. Alikaa Bersheba na kukimbilia Harani Mesopotamia kwa sababu Esau alipanga kumwua kwa sababu ya kuiba haki yake ya mzaliwa wa kwanza. (Fanya muhtasari wa habari)<br>Yakobo alikuwa na umri wa miaka 77 alipoondoka Beer-sheba; alitumia miaka 20 kumtumikia mjomba wake Labani, miaka 33 ya kurudi Kaanani na miaka 7 ya mwisho wa maisha yake Misri.<br>Safari ya kutoka Beer-sheba kwenda Harani likuwa ni maili 500. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yusufu alichukiwa na ndugu zake kwa sababu alikuwa akimwambia Yakobo makosa ya ndugu zake. Yakobo alimpenda sana kwa sababu alikuwa ni mtoto wa Raheli na alizaliwa wakati Yakobo akiwa ni mzee. ***(37: 2)***<br>2. Kanzu yenye rangi nyingi ilikuwa ni kanzu ndefu, yenye mikono mirefu jambo ambalo lilionesha dhahiri mapenzi ya Yakobo kwa Yusufu lakini liliamsha hisia za wivu, chuki na kijicho ndani ya mioyo ya ndugu zake Yusufu. ***(37: 3 & 4)***<br>3. Kwenye ndoto ya kwanza ya Yusufu, ile miganda kumi na moja iliinamia ule wa kumi na mbili, ulikuwa ni unabii kuwa siku moja ndugu zake watamwinamia yeye. Ndoto ya pili ilikuwa pia ni unabii wa kaka zake kumwinamia sambamba na Yakobo (jua) na Lea (mama yake wa kambo) maana Raheli alikuwa amekufa. ***(37: 5-11)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kijana mwota ndoto. | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Wakati wa Mungu ni sahihi kwa kuwa Yakobo aliongozwa kwenye sehemu ile ambayo baadhi ya wachungaji walikuwa wakichunga mifugo yao na mahali ambapo Raheli alikuwa amefika na kondoo zake.<br>2. Yakobo alimfanyia kazi mjomba wake, alitaka kumuoa Raheli, lakini Labani alimdanganya kwa muoza kwanza Lea, binti yake mkubwa. Ilimbidi Yakobo kumtumikia tena Labani kwa miaka mingine saba kabla ya kumuoa Raheli. Akatumikia tena miaka 7 zaidi ***(Mwanzo 29: 15-30)***<br>3. Yakobo alimdanganya baba yake na kaka yake (Esau) na sasa alikuwa anadanganywa na mjomba wake. Yakobo alikuwa amepanda uongo na sasa alikuwa akiuvuna!<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza .**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Wakiwa Harani. |
| **REJELEA SOMO** | Rejea somo ukiwauliza wanafunzi maswali ambayo yatawasaidia kujibu maswali yaliyoulizwa kwenye somo la kwanza la Wakati na Biblia. | Tumia ramani kuwasaidia wanafunzi kupata taswira kwenye fahamu zao kuhusu safari ya Yakobo aliyoifanya kutoka Beer-sheba (kwenye ukanda wa magharibi) kwenda Harani (kwenye mto Frati) ambayo ni Siria ya leo. Unaweza kuvuta hisia zao kwa kuwakumbusha mgogoro unaoendelea leo Mashariki ya Kati kwenye maeneo ya Siria, Yordani na Iraki yote kwamba ni kwa sababu watu wanapendelea kutumainia nguvu za mapenzi yao badala ya kutafuta nguvu ya mapenzi ya Mungu kwenye maisha yao. Ubinafsi wa Yakobo bado unatenda kazi ndani ya maisha ya watu wengi leo – yote haya ni kwa sababu ya ukweli kwamba tulizaliwa katika dhambi! |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Mungu ana mpango kwa ajili ya maisha ya kila mmoja. Pale tunapomwamini Bwana Yesu kama Mwokozi wetu, atatekeleza mpango wake kwetu. Tunalitendea kazi hili kuanzia kile anachotufundisha kwenye Biblia na tunatakiwa kuomba kila siku ili kwamba atuongoze njia zetu katika namna inayompendeza.<br>2. Dhambi ya wivu ni ya kuepukwa kwenye maisha yetu. Biblia inaueleza wivu kuwa 'ni mkali kama ahera' ***(Wimbo ulio bora 8:6)*** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Umuhimu wa kufahamu kwamba kama hatutatubu dhambi zetu na kumwamini Mwokozi kwa wokovu tutavuna madhara ya maisha yetu ya dhambi.<br>2. Uhitaji wa kuhakikisha kwamba kama ni Wakristo na tumetenda dhambi haraka tuungame kwa Bwana Yesu na kupata msamaha wake ***(1 Yohana 1: 9)***, na kugeuka mbali nayo kabla haijaleta madhara katika maisha yetu ambayo yanaweza kutusababishia dhiki. |

| | **B6 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Pili – Maisha ya Yusufu**<br>**Mada – Ndugu aliyechukiwa** | **B6 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Pili – Yakobo na familia yake**<br>**Mada – Wakiwa Penieli** |
| --- | --- | --- |
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 37: 12-36***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Warumi 6: 12***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Dhambi huanza katika namna ndogo kwenye maisha yetu na tusipomwomba Bwana Yesu msamaha dhambi hiyo itakua na kuyaharibu maisha yetu.<br>2. Pale tunapojisikia kuhukumiwa na dhambi zetu ni muhimu sana kuungama mara moja kwa Bwana Yesu. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 32: 1-32***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 32: 11***<br><br>Tunajifunza kuwa :<br>1. Yakobo alimwomba Mungu ulinzi katika hali yake ya hofu.<br>2. Mwisho Yakobo anakabidhi maisha yake kwa Mungu na mara baada ya kukiri kwa Mungu jina lake lilikuwa Yakobo maana yake 'mdanganyifu' na Mungu akambadilisha jina na kuwa 'Israeli' maana yake 'mwana wa mfalme.' |
| **TOA UTANGULIZI** | Rejea habari ya Yusufu na wakumbushe wanafunzi kuhusu mivutano kwenye familia ya Yakobo na sababu zake.<br>Katika ***Mwanzo 27***, Yakobo alimhadaa baba yake Isaka juu ya kumbariki yeye badala ya Esau. Katika somo hili wana wa Yakobo wanamdanganya yeye na kanzu iliyochovywa kwenye damu ya mbuzi. Kuna sababu ya kudhania Yakobo angeliweza kukumbuka hili pale ambapo wanae wanapomdanganya. Uchungu wa hila kwa mara nyingine unagusa maisha ya Yakobo. | Jadili mikutano yoyote ambayo wanafunzi waliwahi kuhudhuria pamoja na watu muhimu yaani viongozi wakubwa. Elezea kuwa katika funzo hili tunafikiria juu ya kukutana na Mungu na matokeo yake kwa Yakobo. Mtu aliyeshindana na Yakobo ***(mstari wa 24)*** alikuwa si mwingine zaidi ya Bwana mwenyewe. Soma ***Hosea 12: 4***. Rejea pia mahali ambapo Bwana (i) anamtokea Musa kwenye kichaka kinachowaka moto; (Kutoka 3: 1-22) (ii) anamtokea Musa katika matukio mawili wakati fimbo yake inageuka na kuwa nyoka na mkono wake kufunikwa na ukoma; ***(Kutoka 4: 1-17)*** (iii) anamtokea Isaya akiwa na ombi na mwitikio wa Isaya; ***(Isaya 6)*** ((iv) anamtokea Sauli njiani kuelekea Dameski. ***(Matendo 9: 1-19)*** Sisitiza kuwa watu wote hawa walikuwa na mikutano muhimu sana na Bwana na uzoefu wa kukumbukwa sana. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Ndugu zake Yusufu walimchukia mno kiasi cha kumtupa shimoni. ***(37: 12-18)***<br>2. Ndugu zake Yusufu walimuuza kwa vipande ishirini vya fedha kwa Waishimaeli, (waliofahamika pia kama Wamidiani) waliokuwa wakielekea Misri. ***(37: 25-28)***<br>3. Baba yake Yusufu, Yakobo anavunjika moyo pale ndugu zake Yusufu wanapomwambia uongo. Wanamwonesha vazi lililochovywa kwenye damu ya mbuzi na Yakobo anachukulia mwanaye amekufa. ***(37: 31-35)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Ndugu aliyechukiwa. | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yakobo alikuwa njiani kurudi kutoka Harani kwenda Kanani na alimhofu Esau kwamba angemuua kama alivyosema miaka ishirini iliyopita ***(Mwanzo 27: 41)***<br>2. Yakobo alituma misafara mitatu ya makundi ya wanyama, 580 jumla, kupatana na Esau. ***(32: 13-21)***<br>3. Yakobo alikaa usiku mzima peke yake Penueli (uso wa Mungu) – uzoefu mkubwa wa maisha yake. Mungu alishika uvungu wa paja lake na alimbadilisha jina kutoka Yakobo na kuwa Israeli ***(32: 22- 32)***<br>4. Yakobo alisikia Esau alikuwa anakuja na watu wapatao 400 kwa hiyo aliigawa familia yake katika makundi mawili ili kwamba ikiwa kundi la kwanza lingekuwa limeharibiwa kundi la pili liweze kukimbia. ***(33: 1-2)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Wakiwa Penieli. |
| **REJELEA SOMO** | Jadili namna Mungu alivyokuwa akishughulika katika habari hii. Waishimaeli ingawa walikuwa hawajui, walikuwa wakitoa usafiri wa bure kwa Yusufu kuelekea Misri kuuzwa kwa Potifa akida wa Farao.<br>Ni katika nchi ya Misri ambapo Mungu alikuwa anakwenda kumbariki sana Yusufu na akawe mtu wa pili katika maamuzi katika nchi ya Misri.<br>Elezea kwamba ***Zaburi 76: 10*** inaonesha Mungu anaweza kufanya ghadhabu ya mtu kumtukuza Yeye na kile kisichomtukuza hukizuia. | Rudia somo hili kwa kuuliza maswali ambayo yatawasaidia wanafunzi kujaza majibu kwenye maswali yaliyoulizwa kwenye somo la pili.<br>Wakumbushe maana ya maneno yafuatayo:<br>Mahanaim ***(mstari wa 2)*** – jeshi la Mungu.<br>Yakobo ***(mstari wa 27)*** – mdanganyifu ama mlaghai.<br>Israel ***(mstari wa 28)*** – aliyeshindana na Mungu ama mwana wa mfalme.<br>Penueli ***(mstari wa 30)*** – uso wa Mungu. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Jadili iwapo wanafunzi wamewahi kuwachukia au kuwaonea wivu wengine ndani ya mioyo yao? Kama ndivyo, wote wanahitajika kuungama dhambi zao kwa Bwana Yesu na kumwomba nguvu ya kuishi bila dhambi. Tazama ***1 Yohana 1: 7***<br>2. Jifunze Mstari Muhimu ***Warumi 6: 12***, na wasisitize wanafunzi kuufanya kuwa kanuni ya kuwaongoza maisha mwao. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Yakobo alikuwa ameachwa peke yake na Mungu ***(mstari wa 24)*** Kama wenye dhambi lazima tuwe na muda binafsi na Mungu ili kusudi tupate wokovu. Kila mmoja anahitaji kukutana na Mungu ili dhambi zake zisamehewe!<br>2. Malaika alishindana na Yakobo ***(mstari wa 24)*** na alimwondolea kiburi chake na unafiki. Ni Mungu pekee anayeweza kufanya hivyo kwa yeyote kati yetu..<br>3. Yakobo alibadilishwa jina. Sote tunahitaji majina yetu kubadilishwa kuwa Wakristo? Waamini? Ndipo tutakuwa tumepata mabadiliko ya mtazamo, msimamo uliobadilishwa mbele za Mungu, mahusiano yaliyobadilishwa, mwenendo uliobadilishwa mbele za Mungu. |

| | B6 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Tatu – Maisha ya Yusufu<br>Mada – Mfungwa mwaminifu | B6 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Tatu – Yakobo na familia yake<br>Mada – Wakiwa Betheli |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 39: 1-6; 19-23***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 39: 21***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ingawa Yusufu alikuwa Misri mbali na nyumbani, aliendelea kuwa mwaminifu kwa Mungu hata katika mazingira magumu sana.<br>2. Macho ya Mungu yalikuwa kwa Yusufu na alikuwa na mpango mkubwa wa baadaye kwa Yusufu. ***(Warumi 8: 28)*** | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 35: 1-15***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Zaburi 37: 7***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Wakati Yakobo anajiandaa kumpokea Esau, alihitaji msaada wa Mungu usiokoma.<br>2. Kama Wakristo tunaweza kutangatanga na kupotea hata kuwa mbali na njia za Mungu kwenye maisha yetu, lakini hawezi kutuacha wala kutupungukia.<br>3. Kama Wakristo, tunahitaji msaada wa Mungu kushughulikia magumu yaliyopita, kushindwa kwetu na majaribu tunayoweza kukumbana nayo baadaye. |
| TOA UTANGULIZI | Jadili makosa ya kusingizia yanavyowaweka watu wasio na hatia magerezani. Elezea jinsi suala hilo lilivyotokea kwa Yusufu.<br>Elezea kwamba katika baadhi ya nchi, leo, waamini wamewekwa vifungoni. Hawapo vifungoni kwa sababu ya chochote walichofanya ila ni kwa sababu wako tayari kuwa waaminifu kwa Mungu, katika kumtumaini na kutii kile walichojifunza kwenye Biblia namna gani waenende kama Wakristo. | Anza Funzo kwa kusisitiza ukweli kwamba wale wote wanaomwamini Mungu wana uhakika wa ulinzi wake – kuna usalama ndani ya Bwana. ***Zaburi 91: 2, 15***; na ***Warumi 8: 31. Zaburi 91*** na ***Warumi 8***, zinaelezea ulinzi huu. Mandiko yafuatayo yanafaa kurejea katika kutoa utangulizi na asili yake: ***Zaburi 91: 2***, 15; na ***Warumi 8: 31***. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yusufu alikuwa ameuzwa na Waishmaeli kama mtumwa kwa Potifa akida wa Farao. ***(39: 1)***<br>2. Mke wa Potifa alisema uongo juu ya Yusufu, alisingiziwa na alitupwa gerezani ***(39: 7-20)***<br>3. Yusufu alikuwa mwadilifu gerezani kiasi cha mkuu wa gereza kumweka kuwa mwangalizi wa wafungwa wote. ***(39: 21-23)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Mfungwa mwaminifu. | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu anamuamuru Yakobo kutimiza kiapo chake alichoahidi miaka thelathini kabla, katika ***Mwanzo 28: 20-22***, na kurudi Betheli.<br>2. Yakobo anaagiza familia yake kuweka mbali miungu ya kigeni na kuosha mavazi yao na walipofanya hivyo wakawa tishio kwa majirani zao ambao ni wamataifa ***(Mwanzo 35: 2-5)***<br>3. Anajenga madhabahu kule 'Betheli' na kumwabudu Mungu aliyemlinda kutoka kwa Esau. ***(Mwanzo 35: 6-7)***<br>4. Mungu anakutana na Yakobo Betheli kwa mara nyingine na anarudia kwa mara nyingine tena agano alilofanya na Ibrahimu na Isaka. ***(Mwanzo 35: 11-13)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Wakiwa Betheli. |
| REJELEA SOMO | Rejea somo kwa kuwauliza wanafunzi kuelezea jinsi Mungu alivyolishinda kusudi la shetani kwenye maisha ya Yusufu na namna Yusufu alivyotoka gerezani kama mtu asiye na hatia, bali ni wa kuaminiwa, mwaminifu na mwajibikaji | Raheli alimwita mwanae Benoni maana yake 'mwana wa uchungu wangu' lakini Yakobo alimwita Benyamini maana yake 'mwana wa mkono wangu wa kuume'. Jadili namna somo hili linavyotoa picha. Kabla ya uzao mwingine, kama ule wa Bwana Yesu kwa kuwa atastahimili uchungu wa msalaba na tena atainuliwa hadi mkono wa kuume wa Mungu mbinguni. Kama vile Betheli ilivyokuwa uzoefu usiofutika kwa Yakobo ndivyo Kalvari ilivyo uzoefu usiofutika kwa Bwana Yesu Kristo na wale wote wanao mwamini Yeye. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Fikiria namna somo hili limetufundisha namna Bwana Yesu anavyoweza kutuhudumia hata katika mazingira ya hatari sana ikiwa tunamwamini na kumtii?<br>2. Kama Mkristo hatuwezi kuepuka majaribu wala magumu. La msingi ni namna gani tunaweza kuitikia pale yanapotujia?<br>3. Fikiria watu wengine kwenye Biblia ambao walifungwa kwa ajili ya imani zao. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Tunapaswa kutafuta baraka za Mungu kwenye maisha yetu kwa kusoma Biblia na kuomba kwa ajili ya maongozi ya kila siku ya Mungu.<br>2. Waambie wanafunzi wajadili kitu gani kilikuwa muhimu sana katika 'uzoefu wa Betheli' kwenye maisha yao.<br>3. Kama Wakristo, tunapokuwa katika magumu, tunapaswa kuhakikisha tunashikilia ile sehemu ya ***Waebrania 13: 5***, - 'sitakuacha wala kukupungukia' |

| | B6 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Maisha ya Yusufu<br>Mada – Kiongozi mpya | B6 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Yakobo na familia yake<br>Mada – Wakiwa Kanaani |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 41: 14-49***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 41: 32***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yusufu alimpa Mungu sifa kwa ule uweza wake wa kutafsiri ndoto mbili na kwa sababu ya unyenyekevu huu, Mungu alimkabidhi majukumu.<br>2. Yusufu alikuwa mwaminifu kwa Mungu siyo tu gerezani bali hata kwenye kasri la Farao na Mungu alikuwa pamoja naye. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 37: 1-36***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Waefeso 4: 31-32***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Upendeleo unaweza kuleta wivu na wivu unaweza kusababisha dhambi yenye madhara kwenye maisha ya watu – mwenye wivu na mwathirika wa madhara ya wivu.<br>2. Ingawa ndugu zake Yusufu waliweza kuishi na dhambi zao kwa miaka mingi, mara Yusufu alipojidhihirisha kwao kabla ya kifo cha baba yake, kukawa na msamaha na upatanisho. ***(Mwanzo 50: 20)*** |
| TOA UTANGULIZI | Kumbuka tena habari na elezea kwamba Mungu alikuwa akifanya kusudi lake ndani ya maisha ya Yusufu.<br>Onesha kwamba kwa sababu ya ushuhuda mzuri wa Yusufu, ***(mstari wa 39)*** alipandishwa cheo kama mtu wa pili katika maamuzi katika nchi.<br>Katika ***mstari wa 42*** pete inaonesha alikuwa ametwaliwa kutoka kwenye nafasi ya utumwa kwenda kwenye nafasi ya mwana wa mfalme; alipewa mavazi ya kitani safi badala ya kanzu iliyochakaa; alipewa mkufu wa dhahabu kuonesha kupanda kwake kwenye mamlaka; na alipewa gari la farasi katika ***mstari wa 43*** kuonesha yeye si mfungwa tena bali mtu anayefurahia uhuru katika ufalme wa Farao.<br>Alitoka kwenye nafasi ya kupuuzwa/kudharauliwa ndani ya shimo alipokuwa na umri wa miaka 17 sasa anakwenda kwenye nafasi ya kuinuliwa/kutukuzwa alipokuwa na umri wa miaka 30. Alikuwa ni kijana mdogo kabisa katika majukumu aliyokuwa nayo! | Itambulishe familia ya Yakobo na hali yao ya sasa.<br>Onyesha historia ya nyuma kwenye somo hili kwa kurejea maandiko mengine ya Biblia.<br>(i) ***Zaburi 56*** – Jadili kuwa kwa Wakristo, Mungu anawaangalia bila kujali namna gani shetani anaweza kuwatumia wengine ili kuwashambulia.<br>(ii) ***Mathayo 5: 43-48; Waefeso 4: 22-32*** Wahamasishe wanafunzi kuukubali na kuupokea mtizamo wa Kristo ulioelezewa na masomo yote katika kipindi cha mateso au upinzani kutoka kwa wale ambao hawampendi Bwana au wafuasi wake ingawa inaweza kuwa ni vigumu sana. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Farao anaota ndoto na Yusufu analetwa kutoka gerezani kutafsiri ndoto. ***(41: 14-16)***<br>2. Yusufu anatafsiri ndoto mbili za Farao – miaka saba ya chakula na miaka saba ya njaa Farao anamweka Yusufu kuwa wa pili kwenye mamlaka na Yusufu anaanza mpango wa kukusanya chakula ***(41: 17-40)***<br>3. Wingi wa chakula ulikuwa mkubwa sana katika miaka saba ya shibe kiasi kwamba haikuwezekana kuwekwa kumbukumbu yake. Ilipofika miaka saba ya njaa kulikuwa na chakula cha ziada kwa ajili ya Wamisri waliokumbwa na njaa na hata maeneo ya mbali ***(41: 46-49, 53-55)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kiongozi mpya. | **Wasilisha Habari ya Biblia.**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yusufu aliota ndoto na alipuuzwa na ndugu zake ***(37: 5-11)***<br>2. Yusufu alipewa na baba yake kanzu au vazi lenye rangi nyingi kama ishara ya upendo kwake lakini jambo hili lilichochea chuki kubwa kwa ndugu zake ***(37: 3-4)***<br>3. Ndoto za Yusufu ziliashiria kwamba ndugu zake 11 na Lea na Yakobo (Raheli alikuwa amekufa) watamwinamia katika siku za usoni.<br>4. Ndugu zake Yusufu walimchukia na walipanga njama za kumuua na kumuuza kwa Waishimaeli (Wamidiani). Bila kujua walikuwa wanatekeleza mpango wa Mungu wa kumuinua Yusufu nyakati za usoni. ***(37: 19-28)***<br>5. Bila aibu ndugu zake walirudisha kanzu ya Yusufu iliyochovywa kwenye damu kwa Yakobo aliyedhania Yusufu alikuwa amekufa na akamwomboleza mwanae kwa kuwa alikuwa anampenda. Yakobo ‘mdanganyifu’ sasa anakuwa ‘mdanganywa’. ***(37: 31-35)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Wakiwa Kanaani. |
| REJELEA SOMO | Waambie wanafunzi wawaze hivi kila mmojawao, yeye ndiye Yusufu na anatakiwa kuandika barua ya kurudi kwa baba yake mzee Yakobo akimwambia juu ya kazi yake mpya! Utaandika nini kwenye barua hiyo? | Rudia Funzo hili kwa kuuliza maswali ambayo yana:<br>(i) Hakikisha wanafunzi wanaelewa kwamba Mungu anashughulika na mazingira yote katika maisha yao na namna ambavyo hapendi warudi tena dhambini.<br>(ii) Hakikisha wanasaidiwa katika kujibu maswali katika Funzo la Nne. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Ni kwa namna gani habari hii inatutia moyo?<br>2. Umejifunza nini juu ya kuwa mtii na mwaminifu kwenye maisha yako ya kila siku?<br>3. Unaweza kutarajia nini kwa njia ya baraka? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Jadili kama ***Waefeso 4: 32*** inafaa kuwa kanuni ya mwongozo katika maisha.<br>2. Kwa kuwa Bwana Yesu haoneshi upendeleo kwa wale walio wema au waovu, kama Wakristo tunalenga kuwatendea kila mtu kwa haki na kwa neema? ***(Mathayo 5: 44-45)*** |

## Maelezo ya Walimu Wanaposaisha Masomo

**Masomo ya Daraja la Tatu**

- Wanafunzi hawawezi kumaliza masomo haya bila kurejelea Biblia na huenda wakalazimika kurejea moja au zaidi ya Usomaji wa Biblia.
- Kuna maswali ya aina mbalimbali pamoja na maneno ya msalaba na gridi za maneno, maneno yanayokosekana, n.k.
- Yameundwa hasa kujibiwa kwa Biblia za matoleo ya NIV, Habari Njema, RSV New King James, Authorized Version na matoleo ya kawaida ya Bibilia ya Kiingereza.
- Lengo letu ni kwamba wanafunzi wote, kwa kutumia Biblia yoyote waliyo nayo, waweze kujibu maswali.
- Alama ishirini zimetengwa kwa kila wiki ambapo kiwango cha juu ni 80 kwa mwezi, pale masomo yanapofanyika kwa usahihi kabisa.
- Daraja la Tatu - Kwa kawaida alama 1 kwa kila jibu inahitajika, kama ilivyoelekezwa.

**Mafunzo ya Daraja la Nne**

- Hili ni toleo gumu zaidi baada ya masomo ya Daraja la Tatu.
- Maswali magumu zaidi na majibu ya kina zaidi yanahitajika.
- Alama ishirini kwa wiki na 80 kwa mwezi, pale masomo yanapofanyika kwa usahihi kabisa, na maswali yanapojibiwa kwa ukamilifu.

**VIDOKEZO VYA USAISHAJI**

Walimu wanatakiwa, kwanza:

- Kupitia kila somo na kutambua majibu sahihi au yasiyo sahihi.
- Kutuza pointi muhimu kama ilivyoelekezwa.
- Kusaisha kila wakati kwa rangi tofauti na KUWEKA TIKI katika kila jibu sahihi.
- Kuingiza jibu sahihi, inapofaa na kurekebisha makosa yoyote ya tahajia, ingawa HAKUNA alama zinazopunguzwa kwa marekebisho haya.
- Kupatia alama chache kwa majibu ambayo usahihi wake sio kamili.
- Kujumlisha alama zote za mwezi na kuandika jumla hiyo kwenye ukurasa wa nyuma katika nafasi iliyotolewa.

Inahitajika kuwa mkarimu na kufanya kila linalowezekana kuwatia moyo wanafunzi waendelee na Mafunzo yao ya Biblia.

Inasaidia, pale inapowezekana kila mwezi kwa mwalimu kuandika neno la kumtia moyo mwanafunzi na kuna nafasi iliyotolewa kwenye karatasi ya somo kwa ajili ya hili kufanyika. Maoni yanaweza kutolewa kuhusu upakaji wa rangi nzuri, unadhifu, alama zilizopatikana, uelewa wa mwanafunzi wa somo, nk.

Tunajaribu kutoa maoni tofauti kadri iwezekanavyo. Maswali, maelezo, ugunduzi, kutia moyo, n.k vyote vinaweza kutumiwa kuleta utofauti. Tunahitaji ubunifu, lakini ni muhimu kuweka mbele masilahi ya mwanafunzi. Ikiwa tunarudia maelezo au swali hilohilo kila mwezi, linapoteza mguso wake kwa wanafunzi.

**DARAJA LA TATU**

**Maoni ya jumla**

“Kazi njema! Ni wazi kwamba ulisoma maswali kwa uangalifu sana. Nimependa sana jibu lako kwa swali la mwisho ambalo lilikuwa na maneno mazuri sana.”

“Halo Yonathani. Asante kwa bidii yako yote. Umefanya vizuri kuweza kupata takriban majibu yote. Nimekujazia majibu ambayo ulishindwa kujibu."

**Maoni ya kiroho**

"Musa alikuwa na wakati mgumu na wana wa Israeli, lakini Mungu hakumwacha atatue shida zote peke yake."

“Yusufu hakusahau kuwa baba yake alikuwa amemfundisha kumpenda Mungu. Alikumbuka hili hata wakati akiwa mbali na nyumbani.”

“Bartimayo alikuwa amedhamiria kufika kwa Bwana Yesu. "Hakukata tamaa kwa kuwa sasa alikuwa anaweza kuona na wakati huu alijua Bwana Yesu alikuwa mtu wa kipekee sana."

**DARAJA LA NNE**

**Maoni ya jumla**

“Seti nyingine ya masomo yaliyojibiwa kwa ubora. Unaonekana kuwa na ufahamu mzuri juu ya habari hizi za Biblia na natumaini kuwa umezifurahia. Asante kwa kutumia muda wako kufanya masomo kwa uangalifu. Ungeweza kuamua kuyapitia juujuu kwa haraka, kwa hiyo natambua bidii yako yote. ”

“Umejaribu vizuri sana, Raheli. Nadhani kwa majibu yako, labda haujaelewa vizuri habari hiyo. Pengine ungejaribu kuisoma tena.”

**Maoni ya kiroho**

"Mifano ya Biblia wakati mwingine huitwa habari za kidunia zenye maana ya mbinguni, au ya kina. Je! Unaweza kufikiria mfano kwenye funzo la tatu una maana gani ya kina? ”

"Stefano alikufa kifo cha kikatili na bado hakuogopa kufa, kwa vile alijua kwamba Mungu yupo na alijua atakuwa na Bwana Yesu Mbinguni."

## Kiambatisho A – Daraja la Tatu Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| **B1** | **Mifano** | **Jirani yangu ni nani?** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/good-samaritan/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-064-good-samaritan/ |
| | | **Mkulima tajiri** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-rich-fool/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/rich-fool/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-greedy-farmer/ |
| | | **Mpanzi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/parable-sower-seed/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/parable-sower/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-049-parable-sower/ |
| | | **Kuwasamehe wengine** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/unforgiving-servant/ |
| **B2** | **Miujiza** | **Maji kuwa divai** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/wedding-cana/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-wedding/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-016-wedding-cana/ |
| | | **Kuponywa kwa kijana** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-020-officials-son/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bible-characters-officials/ |
| | | **Macho ya kipofu kufunguliwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-blind-man/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-blindman-jericho/ |
| | | **Wakoma kumi kuponywa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-072-ten-leprosy/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/hm-ten-leprosy/ |
| **B3** | **Bethania** | **Dada wawili** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-mary-martha/ |
| | | **Huzuni kuwa furaha** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-lazarus1/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-lazarus2/ |
| | | **Safari nyingine** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/jesus-anointed/ |
| | | **Katika mji wa Yerusalemu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/triumphant-entry/ |

## Kiambatisho B – Daraja la Tatu Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| **B4** | **Msalaba** | **Kufa kwake** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-093-mocking-jesus/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-094-pilate/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-095-jesus-led/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-096-jesus-crucifixion/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-097-jesus-cross/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-098-jesus-dies/ |
| | | **Kufufuka kwake** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-101-jesus-resurrection/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-102-appearance-mary/ |
| | | **Kuondoka kwake** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-104-appearance-thomas/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-107-jesus-ascension/ |
| | | **Kurudi kwake** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-ascension/ |
| **B5** | **Wakristo wa kwanza** | **Kuandaliwa na Mungu!** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-ascension/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/pentecost/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/last-supper-jesus/ |
| | | **Kuandaliwa kufa!** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/stephen-martyred/ |
| | | **Kuandaliwa kusikiliza!** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/philip-ethiopian/ |
| | | **Kuandaliwa kwenda!** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/peter-cornelius/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bible-characters-officials/ |
| **B6** | **Yusufu** | **Kijana mwota ndoto** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-dreams/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/josephs-dreams/ |
| | | **Ndugu aliyechukiwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-pit/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-slave/ |
| | | **Mfungwa mwaminifu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-prison/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-prison-dreams/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-slave/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-potiphar/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-baker-cupbearer/ |
| | | **Kiongozi mpya** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-prison-dreams/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-pharaoh-dreams/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-baker-cupbearer/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/pharaoh-dreams/ |

## Kiambatisho A – Daraja la Nne Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| B1 | Mifano | **Wadeni wawili** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-woman-anointing/ |
| | | **Jirani yangu ni nani?** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/parable-good-samaritan/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-064-good-samaritan/ |
| | | **Mtu mpumbavu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-greedy-farmer/ |
| | | **Karamu kubwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/great-feast/ |
| B2 | Miujiza | **Maji kuwa divai** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/wedding-cana/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-wedding/ |
| | | **Kuponywa kwa kijana** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-020-officials-son/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/bible-characters-officials/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-centurion/ |
| | | **Kipofu Bartimayo** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-blindman-jericho/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-blind-man/ |
| | | **Wakoma kumi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-072-ten-leprosy/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/hm-ten-leprosy/ |
| B3 | Bethania | **Nyumbani** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-mary-martha/ |
| | | **Akiwa kaburini** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-lazarus1/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-lazarus2/ |
| | | **Akiwa chakulani** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/jesus-anointed/ |
| | | **Akiwa njiani kwenda Yerusalemu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/triumphant-entry/ |

## Kiambatisho B – Daraja la Nne Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| **B4** | **Msalaba** | **Kufa kwake** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/jesus-crucified/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/jesus-dies/ |
| | | **Kufufuka kwake** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/jesus-alive/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-101-jesus-resurrection/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-102-appearance-mary/ |
| | | **Kupaa kwake** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-ascension/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-ascension/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/pentecost/ |
| | | **Kurudi kwake** |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-ascension/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/last-supper/ |
| **B5** | **Wakristo wa kwanza** | **Stefano** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/stephen-martyred/ |
| | | **Filipo** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/philip-simon/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/philip-ethiopian/ |
| | | **Kornelio** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/peter-cornelius/ |
| | | **Barnaba** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/peter-john-arrested/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/paul-conversion/ |
| **B6** | **Yakobo & familia yake** | **Wakiwa Harani** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jacob-deceives/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jacob-dream/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jacob-returns/ |
| | | **Wakiwa Penieli** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jacob-esau-reunited/ |
| | | **Wakiwa Betheli** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jacob-esau-reunited/ |
| | | **Wakiwa Kanaani** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-dreams/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-pit/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/josephs-dreams/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-slave/ |

© Bible Educational Services 2020

www.besweb.com

Registered Charity UK CIO 1186004

Swahili - 09/2023